# KUISHI KATIKA NYUMBA YA WAKRISTO

## (MWALIMU)



BIBLE STUDIES FOR AFRICAN YOUTH

# KUISHI KATIKA NYUMBA YA WAKRISTO

## (MWALIMU)

Kimeandikwa na Florence G. Chacha, Paul G. Karani na Robert Mutta

**BIBLE STUDIES FOR AFRICAN YOUTH**

Africa Coordinated Curriculum
for Bible Study

Y1-3Ts

Used by permission of International Publications Services

Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

©Copyright, 1990
Baptist Publications House
All Rights Reserved

**2. Omba kwamba wazazi hawatakuwa pingamizi wakati vijana wanapofuata mapenzi ya Mungu kwa kujichagulia wachumba.**

**3. Waombee wazazi wa wanafunzi wako ambao hawajaokoka.**

Sema: "Ni lazima kuwahusisha wazazi katika mipango yote ya ndoa. Ni lazima vijana wawaombe kibali. Wote wanapaswa kuombea jambo hili kama wao ni Wakristo. Mungu atawaonyesha mapenzi yake kama watayatafuta.

"Lakini kunaweza kuwa na shida kama wazazi hao si Wakristo. Huu ndio wakati mzuri wa kuwashuhudia kuhusu mpango wa Mungu kwa maisha yao. Vijana Wakristo wanapaswa kufanya polepole mpango wa ndoa ikiwa ni lazima kwanza wakubaliwe na wazazi wao. Wanastahili kumwomba Mungu awasaidie kusema na kufanya yale yanayomtukuza Mungu. Wanapaswa kumwomba Mungu atumie nafasi hii kuwaokoa wazazi ambao si Wakristo. Inaweza kuwachukua majuma, miezi au miaka kukubaliana, lakini itafaa kama utaanza ndoa yako kwa njia nzuri.

"Mtume Paulo anataja jambo lingine kuhusu nyumba ya Wakristo. Anasema, 'Ninyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu, wasije wakakata tamaa' (Wakolosai 3:21). Hata ingawa wazazi wanapaswa kuheshimiwa, hawastahili kukataa uchaguzi wa watoto wao bila sababu maalum."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Biblia ni mwongozo katika ndoa ya Wakristo. Mtume Paulo anasema katika Wafilipi 1:27 kwamba mwenendo wetu uwe unaostahili injili ya Kristo. Anaendelea kutwaambia katika Waebrania 12:1-2 kwamba tunapaswa kumwangalia Bwana Yesu mwanzilishi na mwenye kuimarisha imani yetu. Mungu na atusaidie tuufikie utimilifu huu."

**KUOMBA**

1. Waombee wanafunzi wako wawatii wazazi wao katika jambo hili muhimu la ndoa.



# YALIYOMO

**SURA** **UKURASA**

1. Mpango wa Mungu kwa Nyumba Kamilifu. . . . . . . . . . . . . .5
2. Mwanadamu Aliamua Kubadili Mpango wa Mungu . . . . . .8
3. Yesu Anamkumbusha Mwanadamu Mpango wa Mungu . 13
4. Maisha ya Mkristo Nyumbani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 17
5. Amri za Mungu kwa Mume . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .21
6. Amri za Mungu kwa Mke . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 25
7. Ushirikiano wa Mume na Mke . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .29
8. Malengo ya Wazazi kwa Watoto Wao . . . . . . . . . . . . . . .34
9. Je! Ni Nani Anayestahili Kuwalea na Kuwarudi Watoto? .38
10. Ibada ya Jamaa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .42
11. Amri za Mungu kwa Mtoto . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 48
12. Je! Nitamwoa Nani? . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .53
13. Je! Ni Nani Anayepaswa Kunichagulia Mchumba? . . . . .58

# HABARI ZA WAANDISHI

Bi. Florence G. Chacha ni mke wa mchungaji huko Nairobi, Kenya, ambaye ana ujuzi wa kufanya kazi na vijana. Amepata elimu ya theologia na kwa sasa yuko katika chuo cha ualimu.

Paul G. Karani ni mwalimu wa masomo ya watu wazima, ambaye pia anawafundisha vijana huko Malindi, Kenya. Yeye ni mshiriki wa Ziyabomu Baptist Church.

Robert Mutta ni mfanya kazi wa Baptist Publications House, Nairobi, katika Idara ya Uhariri. Huwafundisha vijana wa Kahawa West Baptist Church. Anayo shahada ya diploma katika theologia kutoka chuo cha International Baptist Theological Seminary of Eastern Africa. Robert Mutta ni Mtanzania.

**Maelezo**

Sema: "Mungu alisema na Waisraeli walipokuwa wakiiendea Nchi ya Ahadi, katika Kutoka 20:12. Aliwaambia kwamba ni lazima wawatii wazazi wao. Ni lazima mtu ye yote mwenye mamlaka aheshimiwe. Ni muhimu kuwepo na heshima nyumbani. Biblia inatwambia kwamba yule anayewatii na kuwaheshimu wazazi wake ataishi maisha marefu.

"Biblia inawaambia watoto katika Wakolosai 3:20 kuwatii wazazi wao. Je! hii ni pamoja na ndoa? Ndiyo, tunapaswa kuwafahamisha wazazi wetu tunapotaka kuoa. Tunapaswa kuwaomba ruhusa. Kulingana na Mwanzo 24:28, Rebeka hakuifanya siri ndoa yake na Isaka. Alienda haraka na akawaambia jamaa yake. Tunaona katika vifungu vya 50-51 kwamba jamaa yake walikubaliana naye. Soma pia waamuzi 14:1-4 kuona jinsi Samsoni alivyowataka wazazi wake wakubaliane na ndoa yake.

"Je! unakumbuka Kifungu cha Kukumbuka cha sura ya 12? Ni 2 Wakorintho 6:14. Je! ni nani awezaye kukisema?" (Mwambie mmoja wao akisome kama hawakumbuki.)

Sema: "Tunaambiwa wazi kwamba hatupaswi kuunganishwa na wasioamini.

"Je! ni nani anayepaswa kukuchagulia mchumba wa kuoa?" Mwambie mwanafunzi mmoja asome Yeremia 29:11-13. Endelea: "Mungu ana mpango mzuri nawe, anajua kile kinachokufaa. Anakuahidi matumaini kama utamtafuta. Atakuongoza katika kuchagua mchumba kama utamwuliza."

Uliza: "Je! wajibu wako ni nini kwa wazazi katika kumchagua mchumba?" Wape nafasi wale wanafunzi wanaotaka kutoa maoni yao.

wake. Mungu anaweza kutumia jambo hili kuwavuta kwake. Mwamini Mungu na usome Mithali 19:14.

Jamaa nzima wanapaswa kuombea jambo hili kama wazazi ni Wakristo lakini hawakubaliani uchaguzi wa mwanao. Mungu atawaonyesha aliyemchagua.

**KULIFUNDISHA SOMO HILI**

**Utangulizi**

Wasimulie hadithi hii: "Marko na Ruth walitaka kuoana. Walikuwa wamefahamiana kwa miaka mingi na walifanya pamoja kazi ya vijana katika kanisa lao.

"Walipowapasha wazazi wao habari, wazazi wa Marko walikubali, lakini wazazi wa Ruth wakakataa. Wao hawakuwa Wakristo, na hawakutaka binti yao aolewe na Mkristo. Walifikiri kwamba anaweza kusahau baadhi ya mawazo ya kidini kama ataolewa na mtu mwingine.

"'Tutamwomba Mungu awasaidie kuelewa,' Marko akasema. 'Hatutaki kuanza ndoa yetu bila idhini ya wazazi wake.'"

Uliza: "Je! unafikiri ni muhimu kupata idhini ya wazazi? Je! vijana wanapaswa kungojea baraka za wazazi wao? Je! unadhani kwa nini ni muhimu kwa watoto kuwatii wazazi wao? Je! wanapaswa kuwatii hata katika ndoa? Je! wanapaswa kuwatii hadi wapi? Je! hutokea nini kama baraka za wazazi zinatofautiana na mapenzi ya Mungu? Je! kutafanywa nini kama wazazi hawakubaliani na uchaguzi wa watoto wao?" Wape dakika chache za kujadiliana maswali haya. Usitumie zaidi ya dakika tano. Sema: "Hebu tutafute majibu yanayofaa kutoka katika Biblia."



SURA YA KWANZA

# MPANGO WA MUNGU KWA NYUMBA KAMILIFU

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Mwanzo 2:18-24

VIFUNGU VYA LEO: Mwanzo 2:18-24

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja" (Mwanzo 2:24).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawasaidia wanafunzi wangu wajifunze kwamba Mungu aliwapangia mume mmoja na mke mmoja kuoana.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Hakuna

**MSINGI WA SOMO HILI**

Mungu ndiye mwumba wa vitu vyote. Yeye ndiye mwanzo wa vyote vilivyopo. Aliumba kwa mwujiza vitu vyote alivyohitaji kufanyia kazi yake.

Mungu aliumba mbingu na nchi kabla ya kumwumba mwanadamu. Roho wa Mungu ndiye aliyekuwa akipita juu ya nchi. Hatimaye Yesu aliamuru kila kitu kiwepo. Aliumba nuru na giza, nchi kavu na bahari, mimea na viumbe vyenye uhai. Kisha Mungu akaona kwamba hakuna mtu wa kutunza vitu alivyoumba. Ndipo akamwumba mwanadamu kwa mfano wake na ambaye angevitawala vitu vyote alivyoumba. Alimtaka mwanadamu azae, aijaze nchi na kuitiisha.

Bwana Mungu alimwumba mwanadamu kutoka kwa mavumbi ya arthi. Mtu aliyemwumba alikuwa tofauti na wanyama. Aliumbwa kwa njia ambayo Mungu angemtembelea na

kushirikiana na kula naye. Mwanadamu alipewa uhuru wa kuchagua. Alipaswa kuwa mwakilishi na wakili wa Mungu hapa duniani. Bwana Mungu aliangalia kazi yote aliyokuwa amefanya, na alitazama ilikuwa njema sana.

Kisha Mungu akamletea mwanadamu kila mnyama wa msituni na kila kiumbe hai ili avipe majina. Majina aliyowaita mwanadamu ndiyo yaliyokuwa majina yao.

Mwanadamu alipewa vitu hivi vyote, ili avitumie. Lakini vitu hivi vyote havikumfurahisha Adamu. Havingemsaidia wala kushirikiana naye. Mwishowe, Mungu alimwumba msaidizi na akamletea Adamu. Adamu alimwita mwanamke. Alimfanya asikie furaha. Mungu akapanga kwamba mwanamume na mwanamke huyu wawe jamaa ya kwanza. Wangeishi pamoja kama mume na mke.

**KUFUNDISHA SOMO HILI**

**Utangulizi**

Waambie wanafunzi wasomo sehemu ya Utangulizi katika vitabu vyao. Kisha uliza, "Je! Yakobo alijisikiaje alipopewa koti?" Baada ya kujibiwa, sema, "Tutajifunza leo kuhusu Adamu na Hawa. Adamu aliridhika na kuwa mwenye furaha wakati Mungu alipompa Hawa. Hebu tusome Mwanzo 2:18-24." Mwambie mwanafunzi mmoja asome vifungu hivi.

**Maelezo**

Sema: "Mungu alimwumba Adamu baada ya kuumba ulimwengu mzuri na vyote vilivyomo, lakini Adamu alikuwa angali mpweke. Hakuwa na rafiki. 'Bwana Mungu akasema, Si vyema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye' (Mwanzo 2:18). Mungu hakuwa amemaliza kazi yake hata ingawa alimfanyia Adamu mambo mengi. Adamu alihitaji mtu ambaye angetimiza mahitaji ya moyo



zote mbili, kwa sababu kila mmoja atalipwa kwa maovu aliyofanya. Hukumu ya Mungu ni sawa kwa kila mtu.

Biblia inatwambia katika 2 Wakorintho 6:14-15 kwamba tusiunganishwe na wasioamini. Wazazi wasio Wakristo wanaweza kumchagulia mtoto wao mchumba mzuri kulingana na kanuni za ulimwengu huu, lakini pengine mchumba huyo wanayemchagua si Mristo. Ni lazima Wakristo wamfanye Kristo kuwa wa kwanza maishani mwao.

Vijana hawapaswi kuwachagua wachumba kulingana na umbo lao. "Usimtazame uso wake...Bwana haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo" (1 Samweli 16:7).

Soma Mathayo 6:33. Mtu hatafadhaishwa na vitu vingine anavyohitaji anapomtafuta kwanza Kristo. Mungu ana mpango maalumu kwa maisha yetu na amewatayarishia wachumba wale ambao wataoa. Soma Yeremia 29:11-13. Yeye ndiye anayetusaidia kujua yule ambaye tutamwoa. Mungu ndiye anayestahili kutuchagulia wachumba.

Watoto wameambiwa wawatii na kuwaheshimu wazazi wao katika Waefeso 6:1-4. Nao wazazi wameambiwa wasiwachukize watoto wao bali wawalee katika adabu na maonyo ya Bwana. Je! hufanyika nini wakati wazazi si Wakristo, na hawakubaliani na uamuzi wa mwanao? Ni lazima kijana Mkristo awaelezee wazazi wake mchumba aliyechagua kumwoa. Ikiwa hawatakubaliana naye, basi anapaswa kuhakikisha kwamba anampendeza Mungu katika jambo hili. Atapaswa kumwomba Mungu amsaidie kujua iwapo huyo ndiye alimchagulia. Atapaswa pia kuvumilia ili kuwasaidia wazazi wake wakubaliane na uchaguzi wake. Jambo hili laweza kuzuia arusi pengine kwa majuma kadhaa, miezi hata miaka. Lakini ni vyema kukubaliana kwanza na jamaa. Ni lazima avumilie shida hizi za nyumbani kwa roho ya Kikristo akiwaombea wazazi

SURA YA KUMI NA TATU

# JE! NI NANI ANAYEPASWA KUNICHAGULIA MCHUMBA?

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Kutoka 20:12; Yeremia 29:11-13

VIFUNGU VYA LEO: Kutoka 20:12; Yeremia 29:11-13

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Lakini mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo, ili, nikija na kuwaona ninyi, au nisipokuwepo, niyasikie mambo yenu, kama mnasimama imara katika roho moja, kwa moyo mmoja mkiishindania imani ya Injili" (Wafilipi 1:27).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawasaidia wanafunzi wangu wamtegemee Mungu kuwachagulia mchumba, lakini wawatii wazazi wao katika mambo haya yote.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Hakuna.

**MSINGI WA SOMO HILI**

Mungu alimpa Musa Amri Kumi ili mwanadamu aishi kulingana na mapenzi ya Mungu na atimize kusudi la Mungu. Baada ya Mungu kutoa amri za uhusiano wake na mwanadamu, amri yake ya kwanza ya uhusiano kati ya mwanadamu kwa mwanadamu ilikuwa, "Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako" (Kutoka 20:12). Yesu alisema baadaye kwamba, "Ninyi mmekuwa rafiki zangu, mkitenda niwaamuruyo" (Yohana 15:14). Mtume Paulo alizungumzia kuhusu utiifu katika Wakolosai 3:20-21. Alisema pia kwamba wazazi wasiwachokoze watoto wao wasije wakakata tamaa. Amri hii inapaswa kuangaliwa katika pande



wake. Msaidizi huyo angemwonyesha upendo, angemwamini na kujitoa kwake katika maisha ya jamaa. Tunaambiwa katika kifungu cha 21 kwamba Adamu alipata usingizi mzito. Mungu alifanya mwujiza katika usingizi huu ambapo alimwumba mtu mpya aliye tofauti.

"Mungu alimpa Adamu kiumbe hiki kipya kama msaidizi wake. Hivi ndivyo Mungu alivyoanzisha nyumba. Mwanamume na mwanamke huyu walikuwa na wajibu wa kutunzana, kupendana, kuaminiana na kusaidiana maishani.

"Adamu alifurahi sana alipopewa msaidizi huyu. Akasema, '...Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu...' (Mwanzo 2:23). Adamu alijisikia kwamba mwanamke huyu alikuwa sehemu ya mwili wake, naye alipaswa kumpenda jinsi alivyojipenda.

"Watu hawa walitakiwa kuanzisha nyumba ya pamoja ambao haingeweza kuvunjika jinsi ilivyoandikwa katika kifungu cha 24. Wao wangekuwa chombo cha Mungu cha kumjengea unyumba ya kumpendeza."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Mungu aliipangia unyumba uliomfaa Adamu na hata sisi wote. Aliwapangia mume na mke washirikiane katika wajibu wa nyumba yao. Wakristo wanapaswa kumwomba Mungu wanapohitaji mtu wa kuwafariji na wa kuwapenda. Biblia inafundisha katika Mithali 19:14, 'Nyumba na mali ni urithi apatao mtu kwa babaye; Bali mke mwenye busara, mtu hupewa na Bwana.'

"Watu walioona wanapaswa kuijenga jamaa yao jinsi Mungu anavyowaongoza. Wanapaswa kuachwa huru kupanga na kukata mashauri yao wenyewe. Hawapaswi kuwategemea wazazi wao kuwakatia mashauri. Mungu hakubaki katika

bustani ya Edeni kuwaamulia Adamu na Hawa. Soma Mwanzo 2:24. Wao wangekaa pamoja milele na wangekuwa jamaa.

"Hii haiwazuii watu hawa kuwasaidia wazazi wao wawapo na mahitaji. Wanapaswa kuwasaidia, lakini hawapaswi kuwategemea wazazi wao kwa mahitaji yao yote.

"Kuunganishwa kwao kunapaswa kudumu hadi watakapokufa. Yesu amesema katika Mathayo 19:6b, "...Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe."

**KUOMBA**

1. Omba kwamba wanafunzi wako watamwomba Bwana awachagulie mchumba.

2. Waombee wapate kufikiria kwa makini sura zote za kitabu hiki na wapange kukuza jamaa ya Kikristo.

3. Waombee wawe waaminifu katika kuhudhuria masomo ya Biblia.

## SURA YA PILI

# MWANADAMU ALIAMUA KUBADILI MPANGO WA MUNGU

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: 2 Samweli 11:2-27

VIFUNGU VYA LEO: 2 Samweli 11:2-5, 14, 26-27

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Nimekutenda dhambi Wewe peke yako, Na kufanya maovu mbele za macho yako..." (Zaburi 51:4a).



(Waebrania 13:4). Rebeka alikuwa msichana mrembo na angekuwa na wachumba wengi kabla ya ndoa, lakini aliamua kumtii Mungu katika jambo hili muhimu. Ni muhimu kwa kila Mkristo kuishi maisha ya kumtii Mungu ili awe safi mbele zake.

"Mungu ameamuru kwamba, 'Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako' (Kutoka 20:12). Rebeka alipojua kile ambacho matumishi wa Ibrahimu alitaka, alikwenda haraka na kuwaambia jamaa yake. Hakulichukua jambo hili kuwa lake binafsi. Aliwashirikisha jamaa yake.

"Hao wawili wanapaswa kumfanya Kristo kuwa wa kwanza maishani mwao. Rebeka alifanya hivyo kulingana na Mwanzo 24:50-51,58. Yesu amesema kwamba, 'Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa' (Matendo 6:33). Mmoja wenu asome Yohana 12:25."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Tusome pamoja yale ambayo tunaweza kujifunza kutoka kwa somo hili." Wachague wanafunzi kadhaa wasome katika vitabu vyao sehemu ya Mafunzo ya Sura Hii kwangu. Jibu na mjadiliane maswali yo yote ambayo wanayo.

Funga kwa maombi.

**KUOMBA**

1. Omba kwamba wanafunzi wako watatafuta mchumba wa imani sawa na yao.

2. Waombee wapate ujasiri wa kuwa imara kwa uamuzi wanaofanya wakati huu.

unapaswa kumwoa?" Wape muda wa kujibu. Waambie sasa wasome Utangulizi wa somo hili katika vitabu vyao. Kisha sema kwamba watu wenye imani, tabia na mwenendo mmoja ndio wanaostahili kuoana.

Sema: "Hebu tujifunze kutoka kwa Biblia yale ambayo tunapaswa kufanya."

**Maelezo**

Sema: "Kulingana na yale tumeona katika vitabu vyetu, ndoa kati ya Isaka na Rebeka ina funzo muhimu ambalo mtu anapaswa kufikiria anapotaka kuoa.

"Ibrahimu alimwamini Mungu alipomtakia mwanawe mke. Watu wote wanapaswa kuwa na amani kama hii kwa sababu Mungu ndiye anayetupatia mchumba wa maisha." Soma Mithali 19:14.

"Ibrahimu alimtaka Isaka amwoe mtu mwenye imani sawa naye na wa kwao. Hii ndiyo sababu mtume Paulo aliwaambia waamini kutofunganishwa na wasioamini jinsi pasipo ushirika kati ya nuru na giza. Alisema pia kwamba Wakristo wanapaswa kujitenga na uovu, ndipo Mungu atawakaribisha kwa kuwafanya wana na binti zake." (2 Wakorintho 6:14-17)

"Bwana ametuagiza katika Kumbukumbu la Torati 22:10 kwamba tusitumie ng'ombe na punda kwa kulimia jembe moja. Tunaona katika Utangulizi wa vitabu vyenu kuwa Sara alifanya kosa kwa kuolewa na Yohana. Ndoa yao ilivunjika. Hawakuwa na msingi mmoja wa kujengea nyumba yao.

"Naye Bwana alimletea mtumishi wa Ibrahimu msichana mrembo na bikira. Mungu anawataka watoto wake wawe wasafi mbele zake kwa wenzao baada ya kuoa. 'Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi' kwa maana waasherati na wainzi Mungu atawahukumia adhabu'



KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawasaidia wanafunzi wangu wajifunze kwamba watu huteseka wakati wanapokosa kumtii Mungu.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Hakuna

**MSINGI WA SOMO HILI**

Daudi alikuwa mfalme wa Israeli kwa miaka arobaini. Alikuwa amechaguliwa na Mungu kutoka kwa ndugu zake kupitia kwa mikono ya Samweli. Alijawa Roho wa Mungu tangu siku hiyo. Mapenzi ya Mungu kwa mfalme huyu aliyeteuliwa yalikuwa kwamba angekuwa kiongozi wa kiroho aliyetii amri zake. Mungu angemtambua kama kiongozi wa kweli na mfalme wa Israeli.

Daudi alijitoa sana kwa imani, hata akataka kujenga hekalu. Mungu alimkataza asijenge, lakini alikuwa mtawala mwenye uwezo mkuu. Alihakikisha kwamba adui wote wa Israeli wameshindwa na kupewa kazi ngumu.

Mungu alimpenda sana Daudi. Daudi aliokolewa kutoka mikononi mwa Sauli aliyetaka kumwua kwa sababu Mungu alikuwa amemteuliwa kama mfalme wa Israeli.

Daudi alikuwa na wake wengi na alitimiziwa mahitaji yote ya maisha. Lakini Daudi alipuuza mambo haya yote. Siku moja alipokuwa akitembea juu ya dari ya jumba la mfalme, alimwona Bathsheba, mke wa Uria, Mhiti, akiwa anaoga. Uria alikuwa mmojawapo wa maafisa waaminifu wa Daudi waliokuwa vitani. Daudi alimwona Bathsheba akiwa mzuri sana na akataka aletewe. Alizini naye na akapata mimba.

Daudi hakutaka mumewe Bathsheba ajue yale aliyofanya, na akaamuru aje nyumbani kutoka vitani. Alijaribu kumshawishi Uria kwenda nyumbani kwa mkewe ili afikirie kwamba huyu ni mwanawe, lakini hakukubali kwenda huko wenzake wakiwa

vitani. Mwishowe Daudi alipanga kwamba Uria afie vitani ndipo aweza kumwoa Bathsheba.

Dhambi ya Daudi ilileta majonzi. Upanga wa Mungu uliwaangukia wanawe, na Daudi alisikitika sana. Biblia inatufundisha, "Haki huinua taifa; Bali dhambi ni aibu ya watu wo wote" (Mithali 14:34). Daudi alivuna mazao yaliyoletwa na dhambi. Dhambi yake na matokeo yake yalimsumbua maishani mwake mwote.

**KULIFUNDISHA SOMO HILI**

**Utangulizi**

Anza somo hili kwa kusimulia hadithi hii: "Watu walioishi mpakani walisikiliza kwa hamu redioni habari za vita. Kisha kamanda wa jeshi akawatembelea kijijini kwao na kuwaambia kwamba kuna uwezekano kwao kuvamiwa na nchi jirani. Aliwashauri wachukue mali yao wanayoweza kubeba na waondoke mahali hapo.

"Baadhi ya watu walianza kukusanya mali yao na wakaenda katika mji mwingine. Lakini wengine walikataa kuondoka. Hawakuamini kwamba jambo hili litatokea, au vita haitakuwa mbaya jinsi walivyoambiwa.

"Usiku ulipofika, wanajeshi walivamia kijiji hicho huku wakipora na kuharibu mali za watu. Waliwapiga watu hao na kuwaua wengine.

"'Je! kwa nini hatukuondoka wakati tulipokuwa na nafasi?' Wakasema huku wanalia. 'Sasa hivi tungekuwa tumelala usingizi mno.'"

Sema: "Hebu tuone yaliyompata Daudi alipokosa kumtii Mungu na mpango wa Mungu kwa maisha ya Daudi."



Kulikuwa na wasichana wengi warembo huko Kanaani ambao Isaka angeoa, lakini tunaambiwa katika Mwanzo 24 kwamba Ibrahimu alimtaka Isaka kuoa kutoka nyumbani kwao, msichana mwenye imani sawa naye. Ibrahimu alimtuma mtumishi wake amtafutie Isaka mke kaskazini mwa Mesopotamia kule walikotoka. Aliamini kwamba mtumishi wake atamletea mwanawe mke mzuri. Soma Mwanzo 24:1-6.

Kulingana na vifungu 16-28, Bwana alimleta msichana mrembo bikira wakati mtumishi alipoenda kisimani. Alikuwa tayari kumpa maji yeye na ngamia zake.

Mtumishi aliенda nyumbani kwa mtumishi huyo baada ya kuzungumzana kidogo. Hakikisha kwamba umesoma sura yote unapotayarisha somo hili. Tunaona katika vifungu vya 50-61 kwamba Rebeka alimfuata mtumishi yule hadi kwa Isaka naye akawa mumewe. Isaka alimpenda sana Rebeka.

Jinsi Isaka alivyomwoa Rebeka, msichana mwenye imani sawa na yake, ndivyo mtume Paulo alivyowataka Wakristo kuwaoa watu wenye imani sawa na yao, ili waweze kuishi pamoja kulingana na Neno la Mungu.

**KULIFUNDISHA SOMO HILI**

**Utangulizi**

Anza somo hili kwa kusema hivi: "Jambo la kusafiri ulimwenguni limekuwa la kawaida siku hizi, ambapo watu wa sehemu mbalimbali huweza kukutana. Wakati mwingine mwanamume na mwanamke huweza kukutana na kuambiana maneno ya kusisimua. Kisha hufikiri kwamba wamependana, na kupanga arusi mara moja."

Sasa jaribu kujua fikira zao kwa kuuliza: "Je! kuna hatari gani ya kumwoa mtu ambaye mmekutana tu naye na kumfahamu kwa mda mfupi? Je! Biblia inasemaje kuhusu mtu ambaye

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawasaidia wanafunzi wangu wajue kwamba Mungu amempangia kila mmoja mchumba anayefaa wa kukaa naye maishani.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Hakuna

**MSINGI WA SOMO HILI**

Korintho ulikuwa mji wenye utajiri mwingi na kituo cha biashara. Hii ndiyo sababu watu wengi walikutanika huko. Ndipo Paulo aliona kwamba ni mahali pazuri pa kueneza habari njema ya Yesu. Paulo aliufikia mji huu katika safari yake ya pili ya umisheni na akahubiri huko. Paulo aliwafundisha watu jinsi ya kuishi maisha ya Kikristo wakati alipokaa hapo. Hata hivyo, Korintho ulikuwa mji mwovu. Paulo aliona dhambi ya mji huu, na ndipo akaandika mengi kuhusu dhambi ya mwanadamu.

Paulo aliliandika kanisa la Korintho akiwa Makedonia kuhusu kufunganishwa na wasiowaamini. Kulikuwa na shida katika kanisa naye alipaswa kuwaelezea vizuri ujumbe wa injili. Paulo, katika 2 Wakorintho 6:14-7:1, alizungumzia kuhusu kuwa watakatifu mbele za Mungu, wala si kuvutiwa na mambo ya ulimwengu, na jinsi Mungu atakavyowakaribisha walio watakatifu.

Paulo, katika kulinganisha haya na ndoa, alisema kwamba waamini hawapaswi kuwaoa wasiowaamini. Mpango wa Mungu kwa ndoa ulikuwa wazi na halisi. Watu wa imani tofauti hawapaswi kukaa pamoja kama mume na mke jinsi nuru isivyoshirikiana na giza. Hawawezi kuishi pamoja kwa furaha.

Kanisa la Korintho lilikuwa limeacha ukweli wa ndoa, na mtume Paulo aliwaandikia akiwaambia wawe wasafi mbele za Mungu hata katika ndoa. Hakuwataka wachanganyikane na wasiowaamini.



**Maelezo**

Mwalimu, tumia sehemu ya Msingi wa Somo Hili kuongezea somo hili zaidi. Sema: "Daudi alimwona Bathsheba alipokuwa akioga na akamwona kuwa mzuri sana. Aliuliza habari yake, na akaambiwa ni mkewe Uriah. Uria alikuwa afisa mwaminifu aliyekuwa vitani. Kwa hivyo Daudi alimwita Bathsheba na akalala naye.

"Tunaona katika 2 Samweli 11:5 kwamba yule mwanamke alipata mimba na akampelekea Daudi ujumbe kwamba atapata mtoto. Daudi alifanya mpango alipojua kwamba ni kosa kwake kuzini na mke wa wenyewe.

"Daudi aliamuru Uria aje Yerusalemu na kudai kwamba atoe ripoti ya vita. Kisha akamwambia Uria aende nyumbani akidhania kwamba atamwendea mkewe. Ndipo afikiri kwamba mtoto huyo ni wake. Lakini Uria akasema kwamba hawezi kwenda kustarehe nyumbani hali vita vimechacha na wenzake wanapigana.

"Hatimaye Daudi alimlewesha Uria akifikiri kwamba ataenda nyumbani, lakini hakufanikiwa kamwe. Daudi alipoona kwamba ameshindwa, alimwandikia Yoabu barua, na akampa Uria ampelekee. Barua hii ilimshauri Yoabu amweke Uria penye vita vikali. Uria alikufa pamoja na watumishi wengine waaminifu. Daudi alitaka Uria afie vitani ili ionekane kwamba siye aliyemwua.

"Mkewe Uria aliomboleza kifo cha mumewe alipopata habari. Daudi alimwoa baada ya kumaliza kuomboleza na mwishowe akamzalia mwana wa kiume. Soma 2 Samweli 11:26-27.

"Mungu hakumwacha mwana huyo aishi jinsi tunavyosoma katika 2 Samweli 12:15-18. Alikufa kwa sababu ya dhambi hii aliyoitenda Daudi. Mungu hakumpangia Daudi amwoe mkewe

Uria, lakini Daudi alibadili mpango wa Mungu. Dhambi moja ilizusha nyingine hadi alipokuwa na hatia ya uuaji.

"Dhambi ndiyo chanzo cha uharibifu wa mema. Daudi baada ya kifo cha mwanawe anaonekana kuwa mwenye majuto na majaribu mengi. Hebu tuone yale ambayo Mungu anatwambia kutokana na maisha haya ya Daudi."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Mungu alimpa mwanadamu mpango wa kufuata. Alimtaka mwanadamu na mchumba mmoja maishani, lakini mwanadamu amepuuza amri za Mungu. Mwanadamu anafikiri kwamba anafahamu yaliyomema kuliko Mungu. Je! utafuata mpango wa Mungu kwa maisha yako?

"Daudi alifanya uamuzi wake kwa uchoyo, wivu na tamaa. Mungu alikuwa amemtimizia Daudi mahitaji yake yote, lakini Daudi aliona kwamba haitoshi. Je! umeridhika na yale ambayo Mungu amekupatia?

"Mungu alipanga kwamba watu wawili aliowaumba na kuwaweka katika bustani ya Edeni wangeishi pamoja na kufurahia muumbo wake. Wangependana na pia wangempenda Mungu. Maisha yao yangejazwa amani na moyo wa kumtumikia. Lakini hawa wawili walibadili mpango wa Mungu na dhambi ikaingia ulimwenguni. Je! utafanya nini juu ya mpango wa Mungu kwa maisha yako?

"Tunapaswa kufuata mpango wa Mungu na kumtegemea yeye. Mungu hutuonyesha mpango wake tunataka kumfahamu na kusoma Neno lake."

**KUOMBA**

1. Omba kwamba utajitahidi kufahamu na kufuata mpango wa Mungu maishani mwako.



mama zao ili waishi maisha marefu katika nchi ambayo Mungu angewapatia."

Mwambie mwingine asome Waefeso 6:1-3. Sema: "Mungu anatuamuru hivi leo hii, kwamba tuwatii baba na mama zetu ili tuishi vizuri na tuwe na maisha marefu."

Mwambie mwingine asome Luka 2:51, ambao ni mfano wa Yesu wa kuwatii wazazi wake wa hapa duniani.

Sema: "Tujitahidi kuwatii wazazi wetu na kuwaheshimu kwa yote tufanyayo, kwa kumfanya Yesu kuwa msaidizi wetu." Funga kwa maombi.

**KUOMBA**

1. Mwombe Mungu akusaidie uwe na ujasiri wa kuwafundisha wanafunzi wako.

2. Waombee wanafunzi wako waweze kuwaheshimu wazazi wao.

## SURA YA KUMI NA MBILI

## JE! NITAMWOA NANI?

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: 2 Wakorintho 6:14-15; Mwanzo 24; Waebrania 13:4

VIFUNGU VYA LEO: 2 Wakorintho 6:14-15; Mwanzo 24; Waebrania 13:4

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa;, kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza?" (2 Wakorintho 6:14).

wazazi wake. Huwa anaogopa adhabu ambayo atapata. Mtu huonyesha heshima anapojua kwamba mwenzake ana mamlaka, hekima na haki ya kumwamuru jambo la kufanya. Mtu huheshimu afisa wa serikali kwa sababu ya cheo chake. Ni lazima amheshimu mtu huyo. Hii ni tofauti na kumwogopa mtu. Pengine ataogopa kama atavunja sheria, lakini hiyo si heshima."

Uliza: "Je! utii ni nini?" Hakikisha wamesema kwamba ni kufanya kile ulichoamriwa. Inaweza kutokea mara moja, au mara nyingi. Mtu anaweza kutii kwa kwenda kutafuta kuni za kupikia, au kutii amri ya wazazi wake ya kutovuta sigara. Amri ya kwenda kutafuta kuni ilikuwa ya wakati mmoja, hali ya kuvuta sigara iko kila wakati. Unaweza kufanya hivyo kwa kuogopa adhabu, lakini haimaanisha jambo moja."

Sema: "Kuwatii wazazi ni pamoja na kuamua yaliyo mema na mabaya. Agizo hili halibadiliki iwapo wazazi wapo au hawapo. Hivi ndivyo mtoto anaweza kuonyesha kwamba amekua, kwa kuamua yaliyo mema awapo peke yake."

Sema: "Watu wengi siku hizi hufikiri kwamba wao ni werevu kuliko wazazi wao, kwa sababu wazazi wao wamezeeka na hata hawajasoma. Ni kweli kwamba mtu anaweza kuwa msomaji hodari kuliko wazazi wake, au anajua kufanya hesabu kuliko wazazi wake, lakini hiki siyo kipimo cha hekima yao wote. Pengine yule kijana alikuwa na nafasi ya kwenda shuleni kuliko wazazi wake. Lakini wao wamepitia mambo mengi ambayo yamewafundisha mengi ya dhamani. Watoto wanapaswa kuwatii na kuwaheshimu wazazi wao. Mungu amewaamuru wafanye hivyo."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Kutoka 20:12. Sema: "Mungu aliwaamuru hivi wana wa Israeli, wawatii baba zao na



2. Waombee wanafunzi wako wafahamu kwamba watateseka wanapokosa kumtii Mungu. Waombee ili wasimame imara katika Bwana.

### SURA YA TATU

## YESU ANAMKUMBUSHA MWANADAMU MPANGO WA MUNGU

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Mathayo 19:4-6; Marko 10:2-12; Waefeso 5:31

VIFUNGU VYA LEO: Mathayo 19:4-6; Marko 10:2-12; Waefeso 5:31

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:" Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja" (Waefeso 5:31).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawasaidia wanafunzi wangu wafahamu kwamba Yesu alimkumbusha mwanadamu kuhusu mpango wa Mungu wa ndoa.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Hakuna

**MSINGI WA SOMO HILI**

Yesu Kristo alikuja ulimwenguni kutafuta na kuokoa kilichopotea. Alikuwepo wakati wa uumbaji na alifahamu mwanzo wa kila kitu. Soma Yohana 1:1-4. Yesu alishuhudia historia yote na anajua ukweli na kosa.

Yesu kabla ya kwenda Perea alikuwa akifundisha juu ya kuwasamehe wengine. Wanafunzi wake walishangaa aliposema kwamba mtu hapaswi kusamehe tu mara saba bali saba mara sabini. Alikuwa akiwaambia kwamba watu wanapaswa

kusameheana kila wakati. Walistaajabu pia alipowaambia mfano wa mtumishi asiye na huruma. Wote waliona ni vigumu kusamehe. Yesu aliwataka wasamehe kama walitarajia msamaha wa Baba wa mbinguni.

Mafarisayo waliposikia haya, walimwendea na kuanza kumjaribu wakisema, "...Je! ni halali mtu kumwacha mkewe kwa kila sababu?" (Mathayo 19:3) Watu walijua kwamba suluhisho la mwisho ni kuachana kwa sababu kulikuwepo uzinzi na uasherati mwingi. Walikuwa wamejifunza kutoka kwa sheria ya Musa kwamba wana uhuru wa kuwaacha wake zao. Yesu naye akasema kwamba Mungu hajaruhusu tendo hili. Si halali kuachana kwa sababu Mungu aliumba mume mmoja na mke mmoja tangu mwanzo waweze kuishi pamoja. Biblia inafundisha katika Malaki 2:16, "Maana mimi nakuchukia kuachana, asema Bwana, Mungu wa Israeli; naye aifunikizaye nguo yake kwa udhalimu namchukia, asema Bwana wa majeshi; basi jihadharini roho zenu, msije mkatenda kwa hiana."

Hata hivyo, Musa aliruhusu kuachana kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao. "...Musa, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwapa ruhusa kuwaacha wake zenu; lakini tangu mwanzo haikuwa hivi" (Mathayo 19:8).

Wanafunzi wake waliposikia haya wakamwambia, "...Mambo ya mtu na mkewe yakiwa hivyo, haifai kuoa" (Mathayo 19:10). Pengine waliona vigumu kukaa na mke hadi kufa, kisha wakaona kwamba njia pekee ya kuepuka kuachana ni kutooa kamwe. Yesu akawaambia kwamba sio wote ambao watakubali mafundisho haya, lakini "...Awezaye kulipokea neno hili, na alipokee" (Mathayo 19:12).



"Kile Simoni alisikia baadaye ni sauti ya kishindo na uchungu wakati kichwa chake kilipogonga usukani. Alikuwa amegonga mti na bamba la gari likaponyezwa ndani. Jamaa yake walisikia kelele na wakakimbia kwenda kuona kilichofanyika.

"Hakuna aliyehitaji kumkumbusha Simoni kwamba hakumtii nduguye. Alikuwa ameleta hasara ambayo ingegharimu pesa nyingi kutengeneza. Naye alisikia uchungu mwingi kichwani. Je! angesema nini? Je! angefanya nini? Hebu tuone yale Biblia isemayo kuhusu utiifu."

**Maelezo**

Sema: "Hebu tufungue katika 1 Samweli 2:12-36. Kuhani Eli alikuwa na wana wawili ambao walikuwa pia makuhani. Lakini makuhani hawa vijana hawakufanya jinsi Mungu alivyotarajia. Eli aliwaambia wanawe yale Mungu aliwataka wafanye, lakini hawakumtii baba yao mzazi na Baba yao wa mbinguni. Walikuwa walafi, na walikuwa sehemu nono ya nyama zilizoletwa kutolewa kama dhabihu kwa Mungu. Mungu aliwaambia kwamba wote watakufa siku moja kwa sababu ya kutokutii kwao. Tazama sura ya 4, kifungu cha 11. Ningependa mmoja wenu asome kifungu hiki."

Baada ya kusoma sema: "Ilifanyika jinsi mungu alivyosema. Wana hao wawili walikufa siku moja. Dhambi huleta mauti, na kutotii huleta dhambi."

Waambie wanafunzi wafungue katika Waefeso 6:1-2 ambayo ni Kifungu cha Kukumbuka cha leo. Eleza kwamba Mungu atawatuza wote wanaomtii. Uliza: "Je! atawatuza nini?" Mmoja wao asome kifungu cha 3.

Sema: "Tunapaswa kujua kwamba kuwaogopa wazazi wetu si sawa na kuwaheshimu wala kuwatii. Mtoto anaweza kumwogopa baba yake kwamba atamwadhibu kwa kosa alilofanya. Hii siyo kumtii baba yake. Wala hawaheshimu

Warumi 5:19: Dhambi ilikuja duniani wakati mtu mmoja, Adamu, alipofanya dhambi. Adamu na Hawa hawakumtii Mungu, nao uhusiano wao waliofurahia katika bustani ya Edeni ukaisha. Tangu siku hiyo, watu wote wamekuwa watenda dhambi na adhabu ya dhambi hiyo ni kutenganishwa na Mungu, mauti. Lakini hata hivyo, Mungu anao mpango wa kurudisha uhusiano huo. Alimpangia Mwanawe, Yesu Kristo, kufa msalabani (ingawa hakufanya dhambi) kwa ajili ya dhambi za mwanadamu. Yesu alimtii Baba yake, na utiifu wake unawafanya wote wanaompokea kuwa wenye haki.

Tunajifunza katika 1 Samweli 2:12-36 kuhusu kutotii kwa wana wa Eli. Walikufa kwa sababu ya kutotii kwao. Ni vibaya sana kutokuwa mtiifu. Hatupaswi kupuuza jambo hili.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

### Utangulizi

Uliza kama kunaye ambaye atataka kufungua kwa maombi. Simulia hadithi hii. "Simoni alitamani sana kuwa na gari na kuliendesha. Hata aliamua aina ya gari hilo na rangi yake.

"Simoni alifurahi sana wakati nduguye mkubwa alipowatembelea nyumbani kutoka mjini. Alikuwa na gari jipya. Ilimbidi awe na gari kwa sababu anafanye kazi ya uchuuzi. Alimwahidi Simoni kwamba atambeba kabla ya kuondoka, lakini asiingie ndani ya gari hilo mpaka atakapomwita.

"Simoni alilizunguka gari hilo akiangalia kila sehemu yake. Aliugusa mlango na akaona jinsi ulivyo laini. Mkono wake ulishika komeo la mlango, naye akafungua ili atazame tu ndani. Lakini kabla ya kufikiri zaidi alijikuta amekalia kiti cha dereva na anazungusha usukani. Hatimaye aliamua kuachilia breki ili asogeze gari hilo kidogo tu. Kwani, nduguye hangejua!



## KULIFUNDISHA SOMO HILI

### Utangulizi

Anza somo hili kwa kusimulia hadithi hii na kuuliza maswali yafuatayo: "Yohana na Anna waligundua kwamba hawawezi kukubaliana juu ya mambo fulani baada ya kuoana kwa miaka sita. Walikuwa wakigombana mara kwa mara. Hakuelewa kwa nini Yohana hakuja nyumbani hadi usiku wa manane. Yohana naye alilalamika kwamba alitumia vibaya pesa alizompa. Hata watoto walijawa na hofu wakati baba alipofika nyumbani, kwa sababu wazazi hao wangeanza kugombana.

"Yohana alimwambia Anna siku moja kwamba anataka amwache. Alijua kwamba hana furaha maishani, kwa hivyo hakukataa wazo hili. Lakini wakati ulipofika wa kuachana, walitambua kwamba maisha yamekuwa magumu zaidi. Walihitaji vifaa zaidi kuweka katika nyumba zao. Walihitaji mahali pa kuishi na ilikuwa ghali sana. Shida zao zilionekana kama zinaongezeka jinsi muda ulivyopita. Nyumbani hakukuwa mahali pa furaha wala kupumzikia. Walihuzunika sana jinsi walivyokaa peke yao katika nyumba zao.

"Maisha hubadilika sana wakati watu walioona na kukaa pamoja kwa muda wanapoachana. Nyumbani kwao huwa mahali pa uchungu na masikitiko kwa mume na pia kwa mke. Maisha huonekana kama yamefika mwisho. Je! kwa nini watu huendelea kuachana?"

Waongoze wanafunzi wajadiliane juu ya hali hii. Uliza: "Je! Mnafikiri kusudi la Mungu kwa waliooana ni nini? Je! ni kuwataka waishi pamoja kwa muda fulani kisha waachane?" Mwambie mwanafunzi mmoja asome Utangulizi katika vitabu vyao baada ya kumaliza kujibu maswali haya.

**Maelezo**

Sema: "Mwanadamu amekuwa akimkosea Mungu maishani mwake mwote. Mungu anao mpango wa ajabu kwa mwanadamu, lakini mwanadamu anataka kuishi bila mpango wa Mungu. Tunaona katika Mwanzo 1:27 kwamba Mungu alimwumba mume mmoja na mwanamke mmoja ili waishi pamoja kwa upendo, amani na furaha.

"Mwanadamu alionyesha kwamba hastahili mpango wa Mungu. Aliwaoa wake wengi na matokeo yake yalikuwa uchungu na mwishowe kuachana. Jambo hili hufanyika kwa watu wengi siku hizi, lakini Biblia inafundisha kwamba si vyema kuachana. Wawili wanapoachana huwa wangali mume na mke machoni mwa Bwana wakati wangalipo hai. "Mwanamke hufungwa maadamu mumewe yu hai..." (1 Wakorintho 7:39a). Wakati mwingine hutokea kutoelewa na ugomvi kati ya waliooana, lakini hiki si kibali cha kuachana. Yesu anatwambia katika Mathayo 18:21-35 kwamba tunapaswa kusamehe wakati wote.

"Mwanamume na mwanamke ni sawa mbele za Mungu. Tunaona katika Waefeso 5:21-23 kwamba mume ni kichwa cha nyumba jinsi Kristo alivyo kichwa cha kanisa. Kristo Yesu alilipenda kanisa na akajitoa kwa ajili yake. Vivyo hivyo, mume anapaswa kumpenda mkewe na kumtunza. Hapaswi kumchukua kama mtumwa au kitu cha kutendea jinsi atakavyo. Wakristo ni sawa mbele za Mungu. Soma Wagalatia 3:28c.

"Mpango wa Mungu haujabadilika tangu mwanzo, na watu wote wanapaswa kuufuata. 'Mwana mwenye hekima husikiliza mausia ya babaye; Bali mwenye dharau hasikilizi maonyo' (Mithali 13:1)."



mwenendo wa maisha yako. Hii ni amri ya Mungu kwa watoto wake. Wote wanaomfuata wanapaswa kushika sheria zake moyoni mwao na kuzitumia maishani.

Hii huanza wakati watoto wanapowatii wazazi wao. Mtoto asiyetii atakua na kuwa mtu mzima asiyetii mamlaka. Atadharau sheria za nchi na watu wenye mamlaka. Hatamtii Mungu. Mwenendo huu utamletea maisha yenye huzuni na masikitiko. Ni muhimu kwa wanafunzi kufahamu kwamba huwa wanatimiza mojawapo ya amri za Mungu wanapowatii wazazi wao. Huwa wanamtii Mungu.

Hata wazima wanapaswa kuwaheshimu wazazi wao. Tumekwisha jifunza kwamba watu huwa jamaa mpya wanapooana. Wao huwa sasa na wajibu wa kujiamulia na kutenda. Lakini hawana haki ya kutowaheshimu wazazi wao. Watoto wanapaswa kuwa tayari kuwasaidia wazazi wao wawapo wagonjwa au na shida. Pia, watoto wanapaswa kuwatunza wazazi wao wakati ambapo hawajiwezi.

Waefeso 6:2 inasema, "Waheshimu baba yako na mama yako...." Hii ndiyo amri ya kwanza ilioyo na ahadi. Mungu amesema kwamba wale wanaofanya hivyo watafanikiwa na wataishi maisha marefu. Sheria na amri za Mungu hazibadiliki. Nazo zinatuhusu sisi jinsi zilivyowahusu wana wa Israeli siku hizo.

Wakolosai 3:20 inaendelea kuonyesha jinsi Mungu anavyoshughulikia utii wa watoto. Amri hii haipaswi kupuuzwa.

Tunamwona Yesu katika Luka 2:51 akiwa mfano kwetu, jinsi ilivyo desturi yake. Aliwatii Yusufu na Mariamu walipoenda kumtafuta hekaluni. Alionyesha hapa kwamba ni lazima watoto wawatii wazazi wao na kusikiliza wanapoambiwa mema ya kufanya. Soma Mithali 13:1. Kutotii ni dhambi.

3. Omba kwamba kila mwanafunzi ataifanya ibada ya jamaa kuwa sehemu ya nyumba yake atakayoianzisha na mkewe.

## SURA YA KUMI NA MOJA

# AMRI ZA MUNGU KWA MTOTO

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Kutoka 20:12; 1 Samweli 2:12-36; Waefeso 1:9; 6:1-3; Mathayo 19:19; Luka 2:51; Warumi 5:19; 1 Petro 1:14

VIFUNGU VYA LEO: Waefeso 6:1-3; Luka 2:51; Wakolosai 3:20; Mithali 13:1; 1 Petro 1:14

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi" (Waefeso 6:1-2).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawasaidia wanafunzi wangu wajifunze kwamba watoto wanapaswa kuwatii wazazi wao, nao vijana wanapaswa kuwaheshimu.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Kila mwanafunzi atahitaji Biblia.

**MSINGI WA SOMO HILI**

Waefeso 6:1-3: Mungu anawatarajia wazazi wawalee watoto wao kwa upendo na maagizo mema. Ni lazima wazazi wafundishe amri za Mungu, na ni lazima watoto wazikubali na wazifuate. Biblia inafundisha kwamba walio waaminifu na watiifu watatuzwa. Wasio watiifu watakuja juta.

Unapofundisha somo hili wasaidie wanafunzi wako waelewe kwamba kuwa mtiifu sio tu kufuata sheria. Ni kubadili kabisa



**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Pengine utafikiria kwamba ingali mapema kwako kuzifikiria shida hizi. Lakini ni muhimu kupangia maisha yetu na kumruhusu Mungu ayatawale. Ni vizuri kuamua juu ya jambo hili muhimu kabla halijatokea. Nawe utaishi maisha yako ukiwa unafahamu msimamo wako kama Mkristo.

"Je! utajitoa kwa Mungu leo na umwambie akuchagulie mchumba. Mwombe akutayarishe kuwa mume au mke anayestahili. Mwambie kwamba unataka awe sehemu muhimu ya nyumba yako. Mungu atakutimizia hitaji lako na kubariki nyumba yako kama utafanya mambo haya."

**KUOMBA**

1. Omba kwamba utakuwa tayari kuwaongoza wanafunzi wako kujitoa kuwa na ndoa yenye msingi wa Kristo.

## SURA YA NNE

# MAISHA YA MKRISTO NYUMBANI

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Yakobo 1:19-20; Wakolosai 3:8, 12-13, 19-20; Zaburi 19:14; Yohana 13:34; Waefeso 4:15

VIFUNGU VYA LEO: Yakobo 1:19-20; Wakolosai 3:8, 12-13, 19-20; Zaburi 19:14; Yohana 13:34; Waefeso 4:15

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Maneno ya kinywa changu, Na mawazo ya moyo wangu, Yapate kibali mbele zako, Ee Bwana, Mwamba wangu, na Mwokozi wangu" (Zaburi 19:14).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawasaidia wanafunzi wangu wawe Wakristo wema, kwanza nyumbani kwao.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Kalamu na karatasi ya kumpa kila mwanafunzi, ubao na chaki

**MSINGI WA SOMO HILI**

Watu wengi wanaamini kwamba kitabu cha Yakobo kiliandikwa na Yakobo, nduguye Yesu Kristo. Yakobo, mwana wa Zebedayo na nduguye Yohana,aliuliwa na Herodi katika ujana wake. (Matendo 12:2) Kwa hivyo hawezi kuwa ndiye mwandishi wa kitabu hiki. Naye Yakobo, mwana wa Alfayo, (Mathayo 10:3) alikuwa mmojawapo wa wanafunzi wa Yesu lakini haaminiwi na wengi kuwa ndiye mwandishi.

Kwa kuwa Yakobo alikuwa Myahudi, anatupa hekima ya wakati wake ambayo inafaa sana siku hizi.

Hasira huletwa na kutokuwa tayari kusikiliza bali kusema kwa haraka. Yakobo anafundisha katika vifungu hivi viwili kwamba kusikia na kusikiliza, kufikiria kabla ya kusema na kutokuwa mwepesi wa hasira huwasaidia watu kuishi kwa amani na umoja.

Paulo, katika barua yake kwa Wakolosai, alikuwa akiandikia kanisa lililojaa Watu wa Mataifa. Paulo aliwapa mifano inayotokea maishani kwa sababu walikuwa Wakristo wapya. Aliwaambia "wavae" vitu fulani jinsi wavaavyo nguo zao. Soma vitu hivyo katika Wakolosai 3:12-13. Yote yanapaswa kufanywa katika roho ya upendo na kwa kujitoa. (vifungu vya 19-20)

Yohana, mtume wa Yesu Kristo, anatukumbusha kuhusu amri kuu ya Bwana wake, "...Mpendane..." (Yohana 13:34). Upendo huwasaidia watu kukua na kutunzana. (Yohana 13:15)

Nyumba nyingi zimevunjika kwa sababu ya hasira, kutoaminiana, na kukosa upendo. Yakobo anatufundisha kwamba, ni lazima Mkristo atawale hasira yake kupitia kwa mwongozo wa Biblia na uongozi wa Roho Mtakatifu.



haipo nyumbani kwenu. Jadiliana na wazazi wako kuhusu wakati mzuri wa kufanya ibada hiyo. Itakuwa vizuri kama baba wa nyumba ataongoza ibada hii. Mama anaweza akaongoza kama baba hayuko tayari. Kama wazazi wote hawawezi kuongoza, basi Mkristo ye yote anaweza kuongoza."

Uliza: "Je! jamaa wanapaswa kufanya nini nyingine wakati huu wa ibada?" Wape muda wa kujibu na uandike majibu yao ubaoni. Ikiwa wanasita kusema, basi waonyeshe kitabu cha nyimbo ulicholeta. Kwa kweli tunapaswa kumwimbia Mungu sifa wakati wa ibada. Kisha inua Biblia ili wengine wafikirie juu ya kusoma Biblia. Sala inapaswa kuwepo, wakati wa kumsifu Mungu, kumshukuru kwa baraka zake na kuwaombea waliofika na wengine wanao wafikiria. Mnapaswa kuwa na wakati wa kujifunza Neno la Mungu.

Sema: "Ibada ya jamaa inaweza kuwafaidi waliopo kama kiongozi anawafikiria waliohudhuria. Tumia hadithi ya Biblia kama kuna watoto wengi waliohudhuria. Usifanye ibada hiyo kuwa ndefu. Washirikishe katika kuimba, kukariri vifungu na kuomba maombi mafupi. Waulize maswali ili wavutiwe kushiriki.

"Ni muhimu kupanga wakati ambapo jamaa wataacha kila kazi na shughuli na kujiweka mbele za Mungu. Natumaini kwamba utafikiria juu ya kutafutia jamaa yako wakati kama huu." Mwambie mwanafunzi mmoja afunge kwa maombi.

**KUOMBA**

1. Ombea ibada ya jamaa ya nyumba yako. Itakuwa vigumu kufundisha somo hili kama hukutani na jamaa yako.

2. Omba kwamba wanafunzi wako wataanzisha ibada hii nyumbani kwao kama haiko.

unaweza kuwafundisha kwamba Mungu anawapenda nao wanapaswa kumpenda. Hutupatia vyote tulivyonavyo, na kila karama njema hutoka kwake. Unaweza kuwafundisha kuhusu sala, na useme kwamba tunaweza kumwomba Mungu atuongoze na atulinde. Unaweza kuwafundisha watoto jinsi ya kuomba maombi mafupi, na kuwahimiza kuomba kila mara kabla ya kula. Kuna njia nyingi ambazo unaweza kumfundisha mtoto habari za Mungu. Wape nafasi ya kukusaidia kusema njia hizi.

Sema: "Ni muhimu kurudia somo mara nyingi unapowafundisha watoto. Waambie kila siku kwamba Mungu anawapenda, naye anataka wampende, na wanaweza kumwomba wakati wo wote. Waambie yale Mungu anatarajia kutoka kwao mwapo nyumbani. Waambie kwamba kila kitu ulimwenguni kimeumbwa na Mungu hata wao. Waambie mnapokula kwamba Mungu ndiye amewapa chakula hicho na ndiye anayeinyesha mvua ili mazao yapate kukua. Wahakikishie kwamba Mungu huwepo karibu wakati wa raha na shida. Wanapaswa kujifunza kumshukuru Mungu wakati wa raha na shida."

Sema: "Biblia inatwambia kwamba sisi ni nuru ya ulimwengu na tunapaswa kuangaza gizani. Hii ina maana ya kwamba matendo, tabia na maneno anayosema Mkristo po pote alipo yanapaswa kuwa kama ya Yesu Kristo. Anapaswa kuwa mwaminifu, mwenye upendo na tayari kushiriki mambo ya kiroho na kimwili. Hivi ndivyo awezavyo kuwa mfano mwema kwa wengine."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Watu wengi hawajaelewa kwamba jamaa wanapaswa kuwa na wakati wa kukutana pamoja na kumwabudu Mungu. Huu ni wakati muhimu sana wa kukua kiroho kwa kila Mkristo. Pengine itakubudi kuanzisha ibada ya jamaa kama



Ni lazima Mkristo awe mwaminifu kwa Mungu, kwake na kwa wengine. Hawezi kujifanya kuwa mzuri wakati fulani hali mbaya wakati mwingine. Ikiwa inafanyika hivyo, basi mtu kama huyu hajaacha kamwe utu wa zamani wa dhambi.

Ukristo ni dini ya upendo ambayo husisitizwa na mwanzilishi wake, Yesu Kristo. Kutokuwa na upendo huleta shida katika nyumba nyingi. Lakini mtu mmoja akionyesha upendo basi atabadili jamaa nzima.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Waulize wanafunzi waseme baadhi ya mambo mema waliyofanya wiki hii. Yaandike ubaoni wanapoyasema. Omba ukimshukuru Mungu kwa yote mema waliyofanya nyumbani kwao.

Waulize tena waseme mambo ambayo si mema kufanywa nyumbani kwao. Yaandike wanapoyasema na uwaonyeshe tofauti iliyoko. Wape dakika chache za kujadiliana sababu zinazowafanya kufikiria kuwa mambo haya ni mabaya. Hii itakusaidia kuelewa wanafunzi wako na pia kufundisha vyema somo hili.

**Maelezo**

Wagawe wanafunzi wako katika makundi manne. Lipe kila kundi vifungu vya Somo la Leo isipokuwa Kifungu cha Kukumbuka. Wape dakika kumi za kujadiliana yale wanayofikiria kwamba kinafundisha kuhusu maisha ya Mkristo. Kisha wape nafasi ya kutoa ripoti yao.

Sema: "Ni lazima tuanzie nyumbani kuishi kama Wakristo. Nyumba zilizo na amani hujenga makanisa imara. Nawe unaweza kuanzisha amani hii nyumbani kwako. Usiwe

mwepesi wa hasira, kuwa mwaminifu na uipende jamaa yako. Ni lazima tuwe tayari kusikiliza na kuwafikiria wengine."

Sema: "Ukristo wetu unapaswa kuanzia pale tunapoishi. Mungu ana kusudi la kutuweka katika nyumba hizi na kusudi hilo ni kwamba Bwana wetu atukuzwe. Watu walioko nyumbani kwetu watamtukuza Mungu wanapoona maisha ya Kikristo tunayoishi."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Waongoze wanafunzi wajadiliane kuhusu udhaifu wa Yohana katika hadithi ya Utangulizi na waseme yale wanayofikiria. (Watapaswa kusoma Utangulizi huo kama hawajasoma.) Mhimize kila mmoja aseme na adokezee kwa nini anafikiri hivyo.

Wape sasa karatasi na uwaambie waandike udhaifu ulioko nyumbani kwao. Wahakikishie kwamba mtu mwingine hatasoma yale waliyoandika.

Waambie waandike mambo mema yanayofanya nyumbani kwao upande wa pili wa karatasi hiyo na wamshukuru Mungu kwa hayo mema, kisha wamwombe awasaidie waweze kuwaongoza vyema wengine. Waambie warudie pamoja Kifungu cha Kukumbuka.

**KUOMBA**

1. Waambie waombee kimoyomoyo yale waliyoandika. Wahimize wamwombe Mungu awasaidie wawe waaminifu kuombea mambo haya.

2. Mshukuru Mungu kwa wanafunzi wako na jamaa zao.

3. Mwombe Mungu awafanye wawe Wakristo wema nyumbani kwao.



Walipaswa kuzifunga kwenye mikono yao na kuzivaa kwenye uso wao.

"Je! hii inakuonyesha kwamba maneno ya Mungu yalipaswa kuwa muhimu katika maisha ya Waisraeli? Ndiyo, hakuwapangia wayasahau."

**Maelezo**

Soma kwa sauti Kumbukumbu la Torati 6:4-9. Sema: "Walipaswa kuandika maneno ya Mungu kwenye vizingiti vya nyumba zao na kwenye milango kama ukumbusho. Hii inaonyesha jinsi Mungu alivyotaka watoto wajifunze maneno haya na kuyashika maishani. Lilikuwa jambo muhimu kwa Mungu kuona kwamba watoto wamefundishwa. Ukipuuza utakuwa unampuuza Mungu ambapo ni dhambi."

Mwambie mwanafunzi mwingine asome Mithali 22:6. Sisitiza, "Mtoto hatasahau kamwe kama atafundishwa jinsi ya kuishi. Wazazi wanaweza kuwafundisha watoto wao kuhusu ukweli wa maisha wakati wa ibada ya jamaa. Wazazi watawafundisha watoto wao kwamba Mungu anawatarajia wawe waaminifu wa kuweza kutofautisha mema na mabaya. Watu wengine hufikiri kwamba ni vigumu kwa watoto kujifunza kutofautisha mambo na utapoteza wakati ukiwafunza. Lakini ni lazima tuelewe kwamba watoto ni hodari sana kujifunza."

Waambie wanafunzi wafikirie maisha yao hasa walipokuwa wadogo juu ya yale waliyoona, waliyosikia na waliyofanya.

Sema: "Utagundua kwamba ungali unakumbuka baadhi ya mambo yaliyofanyika wakati huo. Kwa hivyo tunapaswa kuwafundisha watoto wetu wakati wangali wadogo jinsi tunavyoambiwa katika Mithali."

Uliza: "Je! unaweza kuwafundisha nini watoto kuhusu Mungu?" Ngojea wajibu. Hakikisha wamesema kwamba

mabadiliko haya walijiunga nao, na kulikuza kanisa. (Matendo 2:46-47)

Tunapaswa kufanya ibada ya kibinafsi. Hii ina maana ya kwamba tunapaswa kumwachia Yesu Kristo atawale maisha yetu. Jamaa ya Kikristo wanapaswa kuabudu pamoja nyumbani kwao. Hatumwabudu Mungu asiyejulikana. Tunamwaabudu Mwumba wa ulimwengu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Tunapaswa kumtolea yaliyomema katika ibada yetu.

**KULIFUNDISHA SOMO HILI**

**Utangulizi**

Uliza: "Je! huwa unafanya nini uwapo na jambo muhimu unalotaka kukumbuka? Je! huwa unaandika maneno machache kwenye karatasi na kuyaweka mfukoni? Je! huwa unasahau kuiangalia karatasi hiyo na kusahau kila kitu?

"Hadithi hii ilisimuliwa juu ya kundi la watu ambao walikuwa na tabia hii. Kama mtu alipewa ujumbe wa kumpelekea mwingine ilimbidi kuchuna jani na kuliweka mdomoni. Angetembea barabarani na jani hilo mdomoni hadi amwonapo mtu huyo na kumpa ujumbe wake. Ndipo alipolitoa jani hilo na kulitupa, ye yote aliyemwona mwenzake na jani mdomoni alijua kwamba hapaswi hata kumsalimia. Salamu zingemfanya mtu huyo asahau ujumbe aliopewa. Marafiki na jamaa wangemsalamia kama kawaida mara tu atoapo jani hilo mdomoni."

Sema: "Waisraeli waliambiwa wampende Mungu kwa moyo wao wote, roho yao yote na kwa nguvu zao zote. Waliambiwa wasisahau amri walizopewa. Mungu aliwaamuru wawafundishe watoto wao maneno haya, na watoto wayarudie wawapo nyumbani, mchezoni, wakipumzika au wafanyapo kazi.



SURA YA TANO

# AMRI ZA MUNGU KWA MUME

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Waefeso 5:26, 28, 33; Wakolosai 3:19; 1 Wakorintho 11:3

VIFUNGU VYA LEO: Waefeso 5:26, 28, 33; Wakolosai 3:19; 1 Wakorintho 11:3

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake" (Waefeso 5:25).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawasaidia wanafunzi wangu waelewe yale ambayo Mungu anatarajia kutoka kwa mume.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Lete kisu, ubao na chaki.

**MSINGI WA SOMO HILI**

Waume wamepewa agizo kuu na Mungu kuliko wanawake. Ni rahisi kutii jinsi wake wanavyoambiwa kuliko kupenda, kama wanavyoagizwa waume. Maandiko yanatwambia jinsi Kristo alivyolipenda kanisa. Upendo wake ulimfanya afie kanisa. Wale wanaofikiria ni rahisi kupenda pengine hawajafikiria kwa makini jambo hili.

Mume anapaswa kumpenda mkewe jinsi anavyojipenda. Paulo anasema, "Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe..." (Waefeso 5:28). Je! mtu huupendaje mwili wake? Sisi huilisha miili yetu. Tunajua kwamba tukila zaidi au tusipopata chakula cha kutosha miili yetu hupatwa na magonjwa. Sisi huiosha miili yetu. Je! mtu

atafananaje kama hachani nywele zake? Je! ni nini kitakachofanyika kama mtu haogi.

Sisi hutunza miili yetu. Hakuna mtu anayenuia kuudhuru mwili wake. Huilinda miili yetu kutokana na hatari yo yote.

Huwa tunapumzisha miili yetu. Je! unaweza kufikiria jinsi mtu anavyoweza kujisikia baada ya kukosa usingizi kwa wiki nzima? Miili yetu inahitaji kupumzika. Kufanya kazi nyingi au ndogo kunaweza kuitatiza miili yetu.

Hizi ni baadhi za njia ambazo sisi hutumia kuonyesha upendo miili yetu. Kunazo nyingine nyingi, na hivi ndivyo Biblia inawaambia waume wawafanyie wake zao. Kama wanawapenda wake zao hawawezi kujinunulia chakula na vinywaji vizuri bila ya kuwafikiria wake zao. Hawawezi kujinunulia tu viatu na nguo. Hawawezi kuwapiga wake zao kwa sababu hivyo ni kama kuipiga miili yao wenyewe. Waume hawawezi kuwatumia wake zao kwa hali ya uchoyo.

Mungu anamtarajia mume ampende mkewe na amlinde na kumtunza jinsi yeye mwenyewe anavyojipenda. Hivi ndivyo Kristo alivyolifanyia kanisa. Mume na mke si watu wawili bali mmoja. Biblia inasema wazi kwamba hao wawili watakuwa mwili mmoja. (Waefeso 5:31) Biblia inaendelea kufundisha kwamba, "Maana hakuna mtu anaye uchukia mwili wake po pote; bali huulisha na kuutunza..." (Waefeso 5:29).

Wake hutendewa kama watumwa au watu wasiofaa katika nyumba nyingi. Wanatarajiwa kufanya kazi kwa bidii, kulala usingizi kidogo, kula chakula kidogo, kuzaa watoto na kutii kila amri ya mume. Lakini kulingana na Biblia ni kwamba waume wanaotarajia mambo haya huwa hawatii amri za Mungu.

Waume wengine huwafikiria wake zao kuwa kama maua nyumbani kwao. Huwataka wakae tu nyumbani, na kuwalisha



## MSINGI WA SOMO HILI

Hapo zamani dini ya Kiafrika ilifuatwa sana maishani. Watu walikula kidini na kuzungumza kidini. Hata kulala nyumbani kwao kulikuwa na msingi wa kidini. Ukristo ni tofauti sana kutoka kwa dini hizo, lakini sehemu hii inahusu pande zote mbili. Kanuni hii ni ya kibiblia.

Agano la Kale linawaonya hivyo watu wa Mungu. Kumwabudu Mungu si kuwepo tu kimwili mahali pa kuabudia. Ni lazima umwabudu Mungu kwa kila hali. Amri za Mungu zinapaswa kutawala maisha yetu. Yale tunayofanya tuwapo nyumbani au mahali po pote ni ibada iwapo tunamtukuza Mungu. Kazi yetu ni ibada kama inamtukuza Mungu. Huwa tunaabudu tunapompa Mungu maisha yetu yote.

Jambo hili hutusaidia kujitayarishia wakati maalum wa kuabudu pamoja nyumbani kwetu. Itakuwa rahisi kwa jamaa katika ibada maalum kama wamezoea kumwabudu Mungu na maisha yao.

Waisraeli waliamriwa kuishi kwa Neno la Mungu. Lilipaswa kuongoza maisha na tabia yote ya watu. Amri za Mungu ziliandikwa kila mahali nazo ziliwakumbusha watu kuishi vizuri. Soma Kumbukumbu la Torati 6:4-9.

Watoto walijifunza jinsi ya kuishi. Wao wangekua na kumcha Mungu kama waliishi na wazazi waliomwabudu Mungu kila siku na pia kwenda mahali pa kuabudia. "Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee" (Mithali 22:6).

Watu wa kanisa la kwanza waliishi maisha kama haya. Wakristo wa kwanza walikuwa watu wa sala na kushirikiana. Waliabudu kama Waebrania walipoenda mahali pa kuabudia. Lakini haikuishia hapo. Walikuwa na ushirika nyumbani mwao ambako walishukuru na kula pamoja. Watu walipoona

"Je! utamwomba Mungu akusaidie kujirudi uwe jinsi anavyotaka? Atakutayarisha uwe mzazi mwema kama utafanya hivyo.

"Hebu tusome pamoja Kifungu cha Kukumbuka." Funga kwa maombi.

**KUOMBA**

1. Omba kwamba utaweza kueleza tofauti ilioko kati ya kuadhibu na kurudi.

2. Omba kwamba wanafunzi wako watakuwa na moyo na nia ya kuwa watu wa marudio mazuri.

## SURA YA KUMI

# IBADA YA JAMAA

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Kumbukumbu la Torati 6:4-9; Matendo 2:46-47; Ufunuo 14:7

VIFUNGU VYA LEO: Kumbukumbu la Torati 6:4-9; Matendo 2:46-47; Ufunuo 14:7

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji" (Ufunuo 14:7).

KUSUDI LA SOMO HILI: Wanafunzi wangu wataelewa jinsi jamaa inavyoweza kuabudu pamoja.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Biblia, kitabu cha nyimbo, ubao na chaki



na kuwataka wasifanye cho chote bali kukaa hapo na kutimiza tamaa za mume. Hii pia si kumpenda mke. Wanawake ni watu pia, na wanapaswa kupewa nafasi ya kuwa jinsi wanavyopaswa kuwa. Wake wanapaswa kutii, lakini kutii kwao kunapaswa kutokana na upendo na heshima wala si hofu.

Mwili wote hutii kichwa kwa manufaa ya mwili wenyewe. Upendo wa bwana humfanya mke atii kwa upendo na jamaa yote watafaidika.

**KULIFUNDISHA SOMO HILI**

**Utangulizi**

Mwite mwanafunzi mmoja aje mbele na umpe kisu ulicholeta. Mwambie ajikate kwenye mkono wake wa kushoto. Angalia jinsi atakavyoitikia. Uliza darasani yule ambaye anaweza kujikata wakati atakapoanza kusitasita. Waulize kwa nini hawawezi kujikata. Wape muda wa kujadiliana, kisha sema:

"Tunaipenda miili yetu sana, kiasi kwamba hatuwezi kuidhuru. Mungu anamtarajia kila mume ampende mkewe jinsi anavyojipenda. Si rahisi kuidhuru miili yetu. Vivyo hivyo, waume wasiwadhuru wake zao. Hebu tujifunze pamoja amri ya Mungu kwa mume."

**Maelezo**

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Waefeso 5:25, 28 na 33. Waulize wanafunzi wafafanue vifungu hivi. Wahimize wafikirie na wazungumzie somo hili la leo.

Uliza: "Je! Kristo alilifanyia nini kanisa?" Wape muda waeleze ufahamu wao kati ya uhusiano wa kanisa na Kristo.

Uliza: "Je! huwa tunaifanyaje miili yetu? Ni kweli kwamba hatupendi kuidhuru kwa sababu ________ (Sema jina lake.) alikataa kujikata." Andika majibu yao ubaoni.

Sema: "Waume wameamriwa kuwapenda wake zao jinsi Kristo alivyolipenda kanisa na wanavyojipenda wenyewe. Cho chote ambacho mume atahitaji anapaswa kujua kwamba mkewe anahitaji pia. Waume wanapaswa kutoa vyote walivyonavyo ili kuwalinda wake zao.

"Mume kama kichwa cha mkewe hapaswi kumfanya mkewe kuwa mtumwa au mali yake. Kichwa huwa hakiamui kuidhuru miguu yake, wala miguu haiwezi kufanya lo lote bila ya kushiriki kwa kichwa."

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Wakolosai 3:19 na 1 Wakorintho 11:3.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Tumesoma kuhusu Yohana na Mariamu katika Utangulizi wa vitabu vyenu. Je! Yohana alimpenda mkewe? Kwa nini unafikiria hivyo?" Ngojea wajibu na mjadiliane.

Sema: "Waume wanapaswa kuwapenda wake zao iwapo wana watoto au hawana, ama kama wana wavulana au wasichana peke yao. Upendo huo haupaswi kutegemea kile ambacho watapata. Je! tunaweza kukata mojawapo ya vidole vyetu kama mkono una vidole vinne? La hasha, huwa tunavitunza na kuvihesabu kuwa sehemu ya miili yetu."

Mwambie mwanafunzi mmoja asome sehemu ya Mafunzo ya Sura Hii Kwangu katika kitabu chake. Waambie waulize maswali kama wanayo, kisha ufunge kwa maombi.

**KUOMBA**

1. Waombee wanafunzi wako wakue ili wawe waume na wake wanaostahili.

2. Mwombe Mungu awasaidie wawe jinsi anavyotaka.



angali anauza mboga. Alistaajabu kusikia sauti ya mama yake nyuma yake akiuliza alipata pesa wapi. Paulo alijua kwamba hataweza kumdanganya. Alimwambia kwamba alichukua kutoka kwa pesa zake.

"Je! mama yake angemwadhibuje?" Ngojea wajibu.

"Je! angemrudi vipi?" Wape muda wa kujadiliana, lakini hakikisha wamesema kwamba angemwambia ni vibaya kuiba. Leo ukiiba senti moja, unaweza kuiba nyingi siku nyingine. Nawe unaweza kuishi maisha ya wizi na kufungwa jela. Au angesema kwamba pesa hizo zilikuwa za karo yake na alikuwa akiziweka ili zitoshee kumrudisha shuleni. Lakini lililo muhimu zaidi, angemwambia kwamba pesa hizo hazikuwa zake na hakuwa na haki ya kuzichukua. Kisha angemwambia Paulo kwamba itambidi kufanya kazi ndipo alipe zile pesa alizochukua.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Marudio si jambo ambalo wazazi wanaweza kuamua iwapo watafanya au hawatafanya. Ni sehemu wa wajibu wao ambao Mungu amewapa wazazi. Wale wanaokosa kuwarudi watoto wao watapaswa kumwambia Mungu sababu ya kutofanya hivyo.

"Marudio huwa hayampendezi mzazi wala mtoto, lakini yatamsaidia mtoto kukua jinsi Mungu anavyomtaka.

"Si watoto tu wanaohitaji kurudiwa. Watu wazima wanahitaji pia. Wakristo wanahitaji kujirudi katika kusoma Biblia, kuomba kila siku na kuhudhuria ibada. Watu wanahitaji kujirudi ili kuacha kunywa na kuvuta sigara. Watu wengine wana magonjwa na hawawezi kula aina fulani ya vyakula. Haya ni mambo machache tu kati ya yale ambayo mtu anapaswa kujirudi.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Wasalimu wanafunzi wanapowasili na uwaongoze kwa maombi. Inua juu fimbo uliyoleta ili kila mmoja aione. Waulize waseme hiyo ni nini na jinsi inavyotumiwa. Waulize kama ni nzuri au ni mbaya. Wape muda mfupi wa kujadiliana.

**Maelezo**

Wagawe wanafunzi wako katika makundi mawili ya watu watano, watano. Wape dakika kumi na tano za kusoma vifungu vya somo la leo na wajibu maswali yafuatayo ambayo umeandika kwenye karatasi uliyowapatia. Je! ni nini maana ya kurudi! kuna tofauti gani kati ya kuadibu na kurudi? Je! ni muhimu kurudi? Je! mzazi anaweza kutamia adhabu gani mtoto anapokosa? Je! anapaswa kutumia marudio yapi?

Waite pamoja watoe ripoti yao. Andika majibu yao ubaoni wanapoyasema.

Eleza kwamba mtu hurudiwa ili kumfanya abadili tabia yake. Kurudi ni kufundisha ili kuwa na kiasi na utiifu. Adhabu ni malipo yanayotolewa baada ya kukosa. Kumwadhibu mtoto kwa kosa alilofanya hakutamfanya atende mema. Anapaswa kuambiwa kwa nini tendo lake ni baya na jinsi anavyopaswa kufanya ili kulirekebisha.

Waambie mfano huu: "Paulo aliona kwamba mama yake alileta mapeni mengi baada ya kuuza mboga. Hata aliona mahali alipoweka.

"'Hatajua kama nitachukua senti moja nikanunue peremende,' aliwaza huku akiiweka mfukoni.

"Paulo alikwenda dukani kesho yake kununua peremende. Alidhani kwamba mama yake hayuko karibu. Alifikiri kwamba





# AMRI ZA MUNGU KWA MKE

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: Waefeso 5:22-23; 1 Peter 3:1-2; Tito 2:3-5

VIFUNGU VYA LEO: Waefeso 5:22-23; 1 Peter 3:1-2; Tito 2:3-5

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu; kusudi, ikiwa wako wasioliamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile Neno" (1 Petro 3:1).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawasaidia wanafunzi wangu wajifunze yale ambayo Mungu anatarajia kutoka kwa wake.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Ubao na chaki

## MSINGI WA SOMO HILI

Sura iliyopita ilizungumzia kuhusu amri za Mungu kwa waume. Biblia haizungumzii tu upande mmoja wa maisha ya Mkristo. Amri za Mungu zinahusu pia wake, na hii ndiyo tutajifunza leo.

Waume wameambiwa wapende na wake wakapewa wajibu mkuu. Wanapaswa kuwatii waume zao. Mtu wa kutii huongozwa au humtii mkubwa wake.

Hii si rahisi, lakini ndiyo njia pekee ya kuleta amani na umoja nyumbani. Ni njia ya kumsaidia mume asiyemwamini kumjia Kristo. (1 Petro 3:1) Kwa hivyo ni muhimu kwa wake kuwatii au kujitoa kwa mumewe, si kwa sababu ya hofu bali kama kwamba anamtii Bwana.

Kumtii Bwana kumefikiriwa kama ni kuwa mnafiki, ambapo ni kujifanya kuwa jinsi ambavyo si kawaida yako. Hakuna mtu ambaye anaweza kumdanganya Yesu, kwa sababu anajua na anaona moyo wako. Kwa hivyo wake hawapaswi kutumia utii kuwatesa waume zao. Wanapaswa kuwatii kama kwamba wanamtii Bwana Yesu. (Waefeso 5:22)

Tendo la kutii si la muda tu. Ni tendo la kufanywa daima maishani. Paulo alimwambia Tito kwamba wazee wa kike hawapaswi kuacha kuwa mifano. Aliandika, "ili wawatie wanawake vijana akili, wawapende waume zao...na kuwa wenye kiasi...(na) kuwatii waume zao wenyewe; ili neno la Mungu lisitukanwe" (Tito 2:4-5).

Wake Wakristo wanapokosa kuwatii waume zao, huwa hawasadiki Neno la Mungu mbele ye waume zao na mbele ya watu wengine. Mwanamke kijana Mkristo anapaswa kuwa na moyo wa kuomba na kujitoa kuwa mke mwema hata kabla ya kuolewa. Naye atakuwa mfano mwema na mwalimu kwa vijana wengine wakati wake unapofika.

Ni muhimu kujitayarisha kuwa mtiifu kabla ya kuolewa. Wanawake hawapaswi kutarajia kupendwa, kusikilizwa na kununuliwa vitu na waume zao kama hawako tayari kuwatii. Waume na wake wana wajibu mkubwa, na wanastahili kuufikiria kabla ya ndoa.

**KULIFUNDISHA SOMO HILI**

**Utangulizi**

Wakaribishe wanafunzi wako na mwimbe wimbo mmoja. Waulize kama wana mahitaji ya kuombea. Waulize wanafunzi wawili au watatu waombee mambo haya.

Waulize vijana wawili waseme mambo ambayo watatarajia wake zao wawatendee. Andika majibu yao ubaoni. Kisha



nyumbani hata hawajui iwapo wanahitaji kuwarudi watoto wao.

Wazazi wengi hawajui kwamba wajibu wao ni kuwaongoza watoto. Pengine hawatajua jinsi ya kufanya hivyo au kuona umuhimu wake. Tendo kama hili huwakuza watoto wasio na adabu, lakini Biblia inafundisha kwamba, "...Bali mwana aliyeachiliwa humwaibisha mamaye" (Mithali 29:15). Ni vyema kusema kwamba huwaaibisha wazazi wote kwa jamii na taifa zima.

Watoto wasio na marudio hukua kuwa watu wazima wasio na marudio. Watakuwa na wajibu wa kuwaongoza wengine, lakini hawataweza kuwaongoza. Watakuwa na kazi za mamlaka, lakini Biblia inaonya, "Waovu wakiongezeka, maasi huongezeka; Bali wenye haki watayatazama maanguko yao" (Mithali 29:16).

Mambo mema hayaji kwa urahisi. Si rahisi kuwarudi watoto. Wazazi wazuri huwapenda watoto wao sana hadi inakuwa vigumu kuwarudi. Ni muhimu kukumbuka kwamba, "Fimbo na maonyo hutia hekima..." (Mithali 29:15). Maadibu yanayofanywa kwa upendo yatafanya maisha ya baadaye ya mtoto kuwa yenye furaha. (Mithali 29:17) Kumrudi mtoto ni kumwonyesha upendo. (Mithali 13:24).

Mwandishi wa Waebrania anaonyesha wazi kwamba Mungu huwarudi watu kwa sababu anawapenda. Watu wazima wanapaswa kustahimili marudio ya Mungu. Kisha watagundua baadaye kwamba yalikuwa mema. Watoto wanaorudiwa na wazazi wao watawatii wazazi wao wawapo watu wazima. (Waebrania 12:5-11)

SURA YA TISA

# JE! NI NANI ANAYESTAHILI KUWALEA NA KUWARUDI WATOTO?

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Mithali 3:11-12; 13:24; 29:15-17; Waebrania 12:5-11

VIFUNGU VYA LEO: Mithali 3:11-12; 13:24; 29:15-17; Waebrania 12:5-11

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe; Bali yeye ampendaye humrudi mapema" (Mithali 13:24).

KUSUDI LA SOMO HILI: Wanafunzi wangu watajifunza kwamba wazazi wanawajibu wa kuwarudi watoto wao.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Fimbo, makaratasi yenye maswali jinsi ilivyodokezwa katika mpango wa kufundishia

MSINGI WA SOMO HILI

Mfano ulioko katika Utangulizi wa vitabu vya wanafunzi ni wakawaida katika jamii yetu. Mambo mengi yamesababisha shida hii. Watoto wameachwa bila mipaka yo yote kwa sababu ya gharama. Wazazi hulazimika kufanya kazi mbali na nyumbani, hali hawana pesa za kutosha. Lakini wao hupokea kile ambacho mtoto huleta bila kuuliza alikotoa. Mtoto huanza kuleta vitu vidogo vidogo nyumbani, lakini vinapokubaliwa huwa ametiwa moyo wa kuiba.

Sababu nyingine ni kwamba wazazi wengi hawana nafasi ya kuwa na watoto wao. Huwa na shughuli nyingi, pia mbali na



waulize wasichana waseme yale ambayo watatarajia waume zao wawafanyie. Yaandike majibu yao ubaoni.

Waulize kama kuna jambo lo lote ambalo wanafikiria halipaswi kuwepo kwenye orodha hizo. Wape dakika kumi za kujadiliana jambo hilo.

Sema: "Unaweza kufikiria kwamba mambo haya yangali mbali, lakini wakati utafika ambapo utakuwa na nyumba yako mwenyewe. Somo lililopita lilizungumzia kuhusu amri za Mungu kwa waume. Sura hii itatufundisha amri za Mungu kwa wake."

**Maelezo**

Waambie wanafunzi wafungue Biblia zao. Wachague wanafunzi tofauti wasome Maandiko ya leo.

Sema: "Biblia inatwambia kwamba wake wanapaswa kuwatii waume zao. Kutii ni kuwa tayari kuongozwa na kuheshimu aliye mkuu. Tuliona kwamba waume ni vichwa vya wake zao.

"Kungetokea nini kama kichwa kingeamua kwenda mahali fulani nayo miguu ikatae kutembea. Je! ingekuaje kama macho yangeona chakula nayo mikono ikatae kuchukua? Tunajua kwamba mwili hautafanya kazi vizuri.

"Je! umewahi kuona nyumba kama hizi? Nyumba hizi zinakosa kitu fulani. Huenda kichwa hakionyeshi upendo au mwili hautii. Mungu amewaamuru wake wawatii waume zao. Hii haipaswi kufikiriwa kuwa na unafiki. Inapaswa kufanywa kama ni kwa Bwana. Yesu anajua na anaona mioyo ya watu. Hata wewe ni mmoja wao.

"Pia si jambo la muda tu. Wake wanapaswa kutii maishani mwao mwote. Hii haitaleta tu amani nyumbani kwao, bali pia itamtukuza Mungu."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Uliza: "Je! ninyi vijana mngependa kuwa na mke kama wa Petro?" Ngojea majibu na uulize kwa nini.

Sema: "Waume watachoshwa haraka na wake wapendao ugomvi. Wanaweza kukosa kupenda kwa sababu ya ugomvi wa wake zao. Baadhi ya waume huanza kulewa kwa sababu ya maudhi ya wake zao.

"Je! kwa nini wasichana hutaka kuwa na nyumba zenye amani? Panga sasa kumtii mume wako. Jambo hili litamfanya akupende zaidi. Unapaswa kujua kwamba hii si amri ya mumeo. Ni Mungu anayewaambia wake watii na waume waonyeshe upendo. Nyumba zinaweza kupata amani na upendo kama amri hizi zinafuatwa."

Wape muda wa kuuliza maswali. Yajibu na kisha ufunge kwa maombi.

**KUOMBA**

1. Mwombe Mungu awasaidie wanafunzi wako wawe waume na wake wema Wakristo.

2. Omba kwamba Wakristo waishio karibu nao watakuwa mifano myema kwao.



amjue Yesu, Mwana wa Mungu na kumpokea kama Mwokozi wa maisha yao."

Mwanafunzi mwingine asome Waefeso 6:4. Sema: "Matokeo huchukiza wakati mzazi anapojaribu kufundisha kwa maneno matupu. Pengine yule mzee aliyeko katika Utangulizi wetu alikuwa amejifunza kwamba pombe ilikuwa imeharibu maisha yake. Aliwataka sana wanawe wajihadhari, lakini alifundisha zaidi kwa matendo yake kuliko maneno."

Mwingine asome 1 Timotheo 3:4-5. Sema: "Kila Mkristo anapaswa kuishi jinsi anavyowaambia wengine waishi. Ni lazima wazazi waishi jinsi wanavyosema kama wanataka watoto watii maneno yao."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Mliona katika vitabu vyenu shida ya watoto fulani ambao hawangeweza kuendelea na masomo kwa sababu ya tabia mbaya. Je! ungependa watoto wako wawe hivyo?" Ngojea wajibu.

Sema: "Nyinyi kama wazazi wa baadaye, ni lazima mfanye yale mnayowaambia watoto wenu wafanye kama mnataka wafanikiwe. Watajifunza haraka kutoka kwa mfano wenu kuliko maneno matupu. Kama hutawafundisha watoto wako kwa mifano, hautakuwa umewaondolea wajibu wao kwa Mungu, bali sasa itakuwa vigumu kwao kufuata mafundisho yake. Turudie tena sote pamoja Kifungu cha Kukumbuka." Funga kwa maombi.

**KUOMBA**

1. Waombee wanafunzi wako waishi maisha kama ya Kristo.

2. Omba kwamba watakuwa mifano myema kwa yote wafanyayo.

"Kulikuwepo na mtu aliyewaambia watoto wake kila siku kwamba wasinywe pombe au aina ye yote ya kileo. Alisema kwamba kulewa huwaletea watu wengi shida, kwa hivyo haikuwa vizuri kunywa. Shida ni kwamba, yeye mwenyewe alikuwa amelewa alipowaambia wanawe maneno haya.

"Siku moja alimpata mwanawe akinywa pombe kwa jirani. Alimpiga kijana huyo akisema kwamba amewakataza wasinywe pombe. Lakini mwanawe hakuacha kunywa. Aliendelea tangu siku hiyo na akamficha babake.

"Je! mtu huyu alikuwa anawafundisha nini watoto wake?"

Wape dakika chache za kujadiliana swali hili kisha uwaambie wafungue Biblia zao. Mwalimu, usijibu swali hili. Litajibiwa tu baadaye katika somo hili. Mwambie mmoja wao afungue katika Kumbukumbu la Torati6:4-9, na mwingine Waefeso 6:4, na mwingine 1 Timotheo 3:4:4-5.

**Maelezo**

Aliyefungua katika Kumbukumbu la Torati 6:4-9 asome sasa. Sema: "Biblia inafundisha kwamba wazazi wanapaswa kumtii Mungu kabla ya kuwafundisha watoto wao kuhusu Mungu. Hii ina maana ya kwamba wanapaswa kuwa mifano myema. Kisha watawafundisha watoto wao po pote walipo. Watapaswa kuwaambia wawapo nyumbani, wakifanya kazi au watembeapo pamoja na wakati wote kunapaswa kuwepo uhusiano mwema kati ya wazazi na watoto kama wanataka kuwafundisha.

"Hitaji la kwanza la mzazi kwa mtoto lapaswa liwe kwamba amheshimu Mungu na kumfanya awe wa kwanza maishani mwake. Wazazi wanaomcha Mungu wanapaswa kumfundisha kila mtoto anayezaliwa kwamba Mungu ana haki ya maisha yake. Atapaswa kutumia maisha yake yote kujua mapenzi ya Mungu na kuyafanya. Wazazi watapaswa kumsaidia mtoto



SURA YA SABA

# USHIRIKIANO WA MUME NA MKE

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Wafilipi 2:1-4; Waefeso 4:2-3

VIFUNGU VYA LEO: Wafilipi 2:1-4; Waefeso 4:2-3

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo" (Waefeso 5:21).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawasaidia wanafunzi wangu wajifunze kwamba ni lazima mume na mke washirikiane nyumbani kwao.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Hakuna

**MSINGI WA SOMO HILI**

Nyumba dhaifu ni mzigo kwa kanisa, jamii na taifa. Baadhi ya wanafunzi wako wanatoka katika nyumba kama hizi. Pengine ni kwa sababu ya pingamizi za kidesturi kati ya wanaume na wanawake au kwa sababu ya kupuuzwa kwa wajibu huo nyumbani kwao.

Mungu alimwumba Hawa kwa sababu aliona kuwa Adamu ni mpweke na anahitaji msaidizi. Mungu alimleta msaidizi huyo mume na mke wapate kufanya kazi pamoja.

Ingefaa kila Mkristo amwoe Mkristo mwenzake. Hii itawasaidia kushinda pingamizi za desturi zao, kwa sababu Wakristo humfanya Kristo kuwa wa kwanza katika mambo yote. Biblia itakuwa mwongozo wao na kanisa mshauri wao.

Baadhi ya watu hujutia uamuzi wao kwa sababu hawakuchagua mtu mwenye malengo sawa nao. Vijana

Wakristo wanapaswa kumfahamu mchumba wao kabla ya kumwoa na waamue jinsi watakavyoshirikiana nao.

Mkristo anapaswa kutumia vifungu vya Biblia kama mwongozo anapomtafuta mchumba. Mahali pazuri pa kuanzia ni Wafilipi 2:1-4. Inatwambia kwamba Kristo ndiye wa muhimu zaidi. Kijana Mkristo anapaswa kujiuliza hivi: "Je! rafiki yangu ananijenga Kikristo? Je! msingi wa upendo wetu ni Kristo? Je! tunafanya na kushuhudia mambo yanayompendeza Kristo?" (2:1)

Pili, Je! tunapenda mambo aina moja? Biblia inasema kwamba, "Ijalizeni furaha yangu, ili mwe na nia moja, wenye mapenzi mamoja, wenye roho moja, mkinia mamoja" (2:2). Je! wote mnataka muishi maisha yapi? Je! mnataka mzae watoto wangapi? Je! mtatumiaje pesa zenu? Je! unatarajia nini ndoa? Je! unatarajia nini kutoka kwa marafiki zako? Ni lazima mume na mke wawe na nia moja kama watashirikiana pamoja.

Tatu, hampaswi kufanya mambo kwa uchoyo. Kulingana na ndoa za Kikristo kila mmoja anapaswa kumfikiria mwenzake. Ikiwa mmoja wenu atataka kufanya ngono (kujuana kimwili) kabla ya ndoa jua kwamba hiyo ni nia ya uchoyo. Hiyo inaweza kukuonyesha ni mtu wa aina gani. (2:3-4)

Lakini pia, watu wawili hawawezi kuwa sawa. Lakini kila mmoja anapaswa kumtii mwenzake kama mnataka kuwa na amani. Mambo haya ni muhimu: upole, unyenyekevu na uvumilivu. (4:2-3) Watu hawa wawili watashirikiana vizuri kama ndoa itakuwa na mambo haya. Ni muhimu kufikiria mambo haya kuliko kiasi cha pesa ambazo mtu anazo. Ni muhimu kuamua yale ambayo kila mmoja anatarajia kifedha na jinsi mtakavyotumia pesa zenu.



mnayoivukia kuimiliki; upate kumcha Bwana, Mungu wako, kushika amri zake zote, na sheria zake, ninazokuamuru, wewe na mwanao, na mwana wa mwanao..." (Kumbukumbu la Torati 6:1-2).

Ni wazi kwamba hawakupaswa kufundisha kwa maneno bali kwa kutenda.

Watoto hujifunza haraka kwa kuona na kufanya. Kwa hivyo, ni vyema kuishi maisha mazuri ya Kikristo nyumbani na kuendelea na mafundisho.

Hii ndiyo Paulo alikuwa akisisitiza katika kitabu cha Waefeso. Aliwaambia waume juu ya wajibu wao wa kupenda na kwamba wake wawatii waume zao, kabla ya kuwapa wajibu wa watoto wao. Kuwalazimisha watoto wafanye yale ambayo hamfanyi nyumbani kwenu ni "kuwakasirisha" (Waefeso 6:4). Hii haipaswi kufikiriwa kama ni kushindwa kuwalea watoto wako. Malezi ni sehemu ya kazi ya Wakristo, lakini ni lazima wahakikishe kwamba imefanywa kwa njia ya upendo.

Kila nyumba ya Wakristo inapaswa kumwakilisha Yesu Kristo. Tabia nzuri ya watoto imetajwa katika 1 Timotheo 3:4-5 kama mojawapo ya hitaji kwa wale ambao watachaguliwa kuwa wachungaji na mashemasi. Hitaji hili halipaswi kuwahusu wahudumu peke yao, bali linapaswa kuwa lengo la kila nyumba ya Wakristo. Mzazi mzuri anapaswa kuwatayarishia watoto wake maisha ya fanaka.

**KULIFUNDISHA SOMO HILI**

**Utangulizi**

Fika mapema ili uandike Kifungu cha Kukumbuka ubaoni au ubandike ukutani karatasi yenye kifungu hiki. Wasalimu wanafunzi wanapofika, kisha anza kwa maombi na urudie kifungu hiki mara nne pamoja nao. Wasimulie hadithi hii:

SURA YA NANE

# MALENGO YA WAZAZI KWA WATOTO WAO

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: Kumbukumbu la Torati 6:1-12; Waefeso 6:1-4; 1 Timotheo 3:4-5

VIFUNGU VYA LEO: Kumbukumbu la Torati 6:4-9; Waefeso 6:4; 1 Timotheo 3:4-5

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: **"Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee" (Mithali 22:6).**

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu yale ambayo wazazi wanatarajia kutoka kwa watoto wao.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Ubao na chaki au kalamu na karatasi kubwa

## MSINGI WA SOMO HILI

Wana wa Israeli walikuwa watumwa kwa miaka mingi. Hawakupewa nafasi ya kwenda shuleni. Hawakuwa na vitabu jinsi tulivyo navyo siku hizi. Mungu alikuwa akiwatayarisha wana wa Israeli kwenda katika Nchi ya Ahadi ambako wangekuwa huru.

Je! ingewezekanaje miujiza ya Mungu na maagizo yake yafikie kizazi hadi kizazi ambacho kingefuata? Ilikuwa wajibu wa wazazi kuhakikisha kwamba watoto wao wamejifunza. Tunaona katika Agano la Kale na Agano Jipya umuhimu wa kufundisha hasa watoto.

Sheria za Mungu zilipaswa kufanywa na wazazi kisha kufundishwa watoto wao. Musa aliwaagiza Waisraeli kuhusu amri za Mungu. "...mpate kuzitenda katika nchi ile



## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Wafilipi 2:1-4.

Sema: "Maandiko haya yanatwambia kwamba maisha yetu huwa imara tunapoishi ndani ya Kristo na upendo wake hutufariji. Kristo atatusaidia kusuluhisha shida zetu kama tutamwacha atawale jamaa zetu. Tutaonyeshana upendo na wema iwapo tutakubali kushiriki katika Roho wa Bwana."

**Maelezo**

Sema: "Ni lazima kuwa na wakati wa maombi katika nyumba za Wakristo. Hasa wakati ambapo jamaa wanatafuta hekima itokayo juu. Mume na mke wanapaswa kuanzisha jambo hili, na kuwahusisha watoto wanapopatikana katika jamaa yao. Wakati huu utakuwa muhimu kwa jamaa nzima. Wazazi watapata nguvu na msaada wa shida zao. Watoto watajifunza kule ambako watapata msaada wapatapo shida maishani mwao. Watajifunza kwamba maombi ni ya muhimu kwao ikiwa ni ya muhimu kwa wazazi wao.

"Hii haichukui nafasi ya wakati wa kimya na Mungu ambao unapaswa kufanywa na kila mmoja. Kila mmoja anapaswa kuwa na wakati wa maombi mafupi ya kumwezesha kukua kiroho. Wakati huu ni wa kumsaidia yule anayeomba kumkaribia Mungu kwa sala na kusoma Biblia. Ni vigumu kwa mume na mke kuishi pamoja kwa amani kama hawamjui Yesu Kristo na hawajaamua kumfuata. Wanaweza tu kuenenda naye wanapoamua kuwasiliana naye kila siku."

Sema: "Kristo huwapa waume na wake furaha wawapo na nia moja, na kufurahia pendo moja na kuenenda katika malengo na tumaini moja. Hawapaswi kufanya jambo lo lote kwa uchoyo au tamaa au majivuno. Wanapaswa kuwa wapole

wakiwafikiria wengine jinsi wanavyojifikiria wenyewe. Njia moja ya kufanya hivyo ni kufahamu yale yanayompendeza mwenzako na kumhimiza kwayo."

Sisitiza yale ambayo Waefeso 4:2-3 inawambia kwamba tunapaswa kuwa wanyenyekevu, wapole na wavumilivu. Tunapaswa kuonyesha upendo kwa kustahimiliana. Tumia sehemu ya Msingi wa Somo Hili kuongezea mafundisho mengine muhimu.

Sema: "Wakati kuwapo na shida katika jamaa, mume na mke wanapaswa kukaa pamoja na kuzungumzia shida hiyo. Kisha watafute chanzo cha shida hiyo na njia za kuisuluhisha. Mabishano hayapaswi kuwa sehemu ya mazungumzo hayo kwa sababu hayamtukuzi Mungu. Ni lazima maswali yaulizwe kwa upole na kujibiwa vizuri hata ingawa mambo ni mabaya sana. Kisha mtapaswa kumshukuru Mungu mnapopata suluhisho."

Sema: "Ni lazima pia nizungumzie juu ya wivu. Wivu uko ndani ya kila maumbile ya mwanadamu na umeiletea jamaa nyingi shida. Nyinyi kama mume na mke mnapaswa kujilinda na ovu hili. Usifanye jambo lo lote ambalo litamfanya mwenzako aone wivu."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Waume na wake wanapaswa kuheshimiana. Kila mmoja ana kipawa na ujuzi tofauti ambao unaweza kusaidia kumletea mwenzako furaha. Kila mmoja ni wa muhimu katika jamaa, na kila mmoja husaidia kutenda wema kwa jamaa nzima.

"Katika ulimwengu huu wa sasa watu hujitahidi kutafuta vitu wanavyotaka na kuhitaji. Mara kwa mara wao hufanya kazi kwa saa nyingi ndipo wavipate. Hatimaye huwa wachovu na kusema maneno makali. Je! kuna njia nzuri zaidi? Je! wanaweza kuwa na amani na furaha katika jamaa?



"Ndiyo, jamaa iliyounganishwa katika upendo wa Kristo na kwa ajili ya mwenzake hupata amani na furaha. Nao wataweza kustahimili hata wakati wa shida. Hili si jambo ambalo linaweza kununuliwa na pesa. Linaweza kupatikana tu katika Yesu Kristo na kwa kuenenda naye.

"Je! utaamua leo kumfanya Yesu kuwa msingi wa nyumba yako? Atakusaidia na kubariki juhudi zako za kujenga nyumba ya Kikristo.

"Ni lazima mume na mke waandike malengo ya maisha yao ndipo wafanikiwe kushirikiana pamoja. Kisha wanaweza kupanga jinsi watakavyo yatimiza pamoja. Mwombe Mungu akusaidie kufanya hivyo."

**KUOMBA**

1. Iombee jamaa yako na uombe kwamba wewe na mwenzako mtajitahidi kushirikiana.

2. Waombee wanafunzi ambao hawatoki katika jamaa za Wakristo. Itakuwa vigumu kwao kuelewa somo hili. Mwombe Mungu awasaidie kuelewa.

3. Waombee wanafunzi wako wajitoe kuchagua rafiki Mkristo na wajenge nyumba zao juu ya Yesu Kristo.